Jumanne Mei 7, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0579911

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


Ni huzuni

DK. MENGI

Sauti ya kumkosa kila kona

UKURASA 13

**UHUSIANO**
Rais John Magufuli, amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Idara ya Afrika wa Shirika la Fedha la...

UKURASA 2




**MFUNGO RAMADHANI**
Waumini wa dini ya kiislam leo wanaanza mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na Kadhi Mkuu wa Tanzania, Abdallah Mnyasi...

UKURASA 4

# Umati waupokea mwili wa Dk. Mengi

• **Licha** ya mvua wazuia barabara, watandika khanga barabarani gari lililobeba mwili lipite na kurusha maua... *Endelea ukurasa 2*

**KWAHERI BABA...**





Umati wa waombolezaji wakiwa wameuvamia msafara wa gari lililobeba mwili wa marehemu Dk. Reginald Mengi, katika Barabara ya Kawawa, eneo la Kinondoni Mkwajuni, jijini Dar es Salaam jana. **Picha ndogo kushoto;** watoto wa marehemu Regina na Abdiel. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Maelfu waliotumbuliwa vyeti feki warejeshwa

UK. 10

**MICHEZO** **SIMBA YAREJESHA 'DO OR DIE' BARA** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Wananchi wa Kijiji cha Nkuu Sinde, Kata ya Machame Mashariki katika Wilaya ya Hai, wakiendelea na kazi ya kuandaa kaburi ambalo atazikwa aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP Ltd, Dk. Regnald Mengi nyumbani kwake Kisereni. **PICHA: GODFREY MUSHI**.

# Mapokezi ya kifalme

**Na Waandishi Wetu**

NI MAPOKEZI YA KIFALME: Hivyo ndivyo unavyoweza kusimulia namna umati ulivyojitokeza kushuhudia msafara wa mwili wa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, uliowasili jana na kupumzishwa kwenye Hospitali ya Jeshi Lugalo jijini Dar es Salaam.

Maelfu ya watu jana walijitokeza kwa wingi kwenye njia zote ulipopita msafara wenye mwili huo kuanzia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), huku wengine wakishindwa kujizuia na kuangua vilio.

Mwili wa Dk. Mengi ulitolewa kwenye jengo uwanjani hapo majira ya saa 10:22 jioni na baada ya sala, msafara huo ulianza kuelekea Hospitali ya Jeshi Lugalo ambapo maelfu ya watu walisimama barabarani kupokea.

Msafara huo ulitoka Airport na kupitia barabara za Vingunguti, Buguruni, Karume, Ilala, Kigogo, Magomeni (Kanisa Katoliki), Morocco, New Bagamoyo Road, ITV, Mwenge hadi hospitalini Lugalo ambako uliwasili majira ya 12: 30 jioni.

Majira ya Saa 10:57 jioni, msafara huo ulikuwa barabara ya Tazara na ulipofika eneo la Buguruni idadi ya watu iliendelea kuongezeka na kusababisha msafara huo wakati mwingine kusimama kwa muda.

MSAFARA WASIMAMA

Maeneo ya Buguruni Sheli, Buguruni Sokoni wananchi waliojitokeza walishindwa kujizuia na kulazimika kuuzuia msafara huo ili waweze kutoa heshima zao kwa Dk. Mengi, ambaye amesaidia maelfu ya watu wakati wote wa uhai wake.

Kutokana na hali hiyo, Kamanda wa

INAENDELEA UK. 8

## ...Mwinyi: Kifo chake pigo kwangu, maelfu kwenda Hai

**Na Waandishi Wetu**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, amesema kifo cha Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi ni pigo kwake binafsi kama ilivyo kwa Watanzania wengine na familia ya marehemu.

Jana, Rais mstaafu Mwinyi alifika nyumbani kwa marehemu kuomboleza kifo cha Dk. Mengi na kumwelezea kuwa alikuwa mtu mkarimu aliyependa watu.

"Dk. Mengi alikuwa mkaribu sana, siyo mkarimu wa mali tu bali wa fikra, mkarimu kwa watu, mkarimu wa mawaidha, alikuwa kila kitu chake ni sawa na chetu sote leo ameondoka tutamkumbuka," alisema.

Mwinyi ambaye alikuwa ameambatana na mke wake, Sitti alisema kuwa amefika na familia yake siyo kumsifu Dk. Mengi bali kutoa pole kwa wafiwa wote.

"Sisi tuko pamoja na familia, Dk. Mengi na mimi tulikuwa karibu sana, kuondoka kwake ni pigo kwangu kama ilivyo kwa familia yake na sote rafiki zake," alisema.

**WAOMBOLEZAJI 5,000 KUWASILI HAI**

Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amesema taarifa za awali mpaka sasa zinaonyesha kuwa idadi ya waombolezaji wanaotarajiwa kufika katika Kijiji cha Nkuu Sinde, Kata ya Machame Mashariki mahali ambako Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Regnald Mengi, atazikwa nyumbani kwake Kisereni ni zaidi ya watu 5,000

Baada ya kufika nyumbani kwa marehemu Dk. Mengi jana asubuhi kwa ajili ya ukaguzi wa maandalizi ya mazishi hayo na kujiridhisha kuhusu maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kukaa viongozi waandamizi wa serikali, viongozi wa dini, wanasiasa, jumuiya ya wafanyabiashara nchini na watu mashuhuri, Ole Sabaya alisema wanataraji kupokea idadi kubwa ya watu kuanzia kesho (Jumatano).

Ole Sabaya ambaye alikuwa ameongozana na wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo, alifika nyumbani kwa Dk. Mengi eneo la Kisereni saa 5:02 asubuhi na kupokelewa na kiongozi wa itifaki wa familia ya Dk. Mengi, Wilfred Mushi.

"Tumefika hapa nyumbani kwa mzee Regnald Mengi kama kamati ya ulinzi na usalama, tumekutana na familia, tumekuja kuangalia maandalizi ya safari ya mwisho ya mzee wetu Regnald Mengi na kama mlivyoona tumekuja kuangalia namna maandalizi mbalimbali yanavyoendelea, tunategemea tutapokea watu wengi sana, tutapokea viongozi mbalimbali, tutapokea wafanyabiashara ndani ya Wilaya ya Hai, tutapokea wadau wengine wengi na wananchi kwa ujumla.

"Kwa hiyo tumekuja kuangalia maandalizi kwa ujumla hasa kwenye barabara hii ya kuja hapa (Nkuu Sinde-Kisereni), lakini pia tumekutana hapa tayari maandalizi ya uchimbaji wa kaburi yanaendelea sehemu ambapo ni makaburi ya familia ya mzee Mengi; ambapo watamweka kwenye makao yake ya mwisho. Maandalizi yako vizuri."

Zaidi Ole Sabaya alisema: "Nimeelekeza hapa na nitaacha hapa baadhi ya viongozi wenzetu wa kamati ya ulinzi na usalama watakuwa wanaendelea na maandalizi madogo madogo wakishirikiana na familia, lakini wakati huo huo tukiwasiliana na wengine wa Dar es Salaam kuona kwamba hizi ratiba zote zina kuwa compatible (zinakwenda sawa sawa).

TENDA YA UJENZI WA KABURI

INAENDELEA UK. 8

# JPM, kigogo wa IMF wateta Dar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Idara ya Afrika wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Abebe Aemro Selassie Ikulu jijini Dar es Salaam.

Baada ya mazungumzo hayo, Selassie alisema aliomba kukutana na Rais Magufuli ili kuzungumzia masuala mbalimbali yanayohusu uhusiano wa muda mrefu kati ya Tanzania na IMF na jinsi shirika hilo linavyoshiriki katika kutoa ushauri wa kiuchumi.

Selassie alimpongeza Rais Magufuli na Serikali anayoiongoza kwa juhudi kubwa zinazofanywa kuwekeza katika miradi mikubwa ikiwemo miundombinu itakayopunguza gharama za nishati ya umeme.

Kuhusu kuvuja kwa taarifa za ukuaji wa uchumi, Selassie alisema IMF itatuma timu ya wataalamu wake itakayokutana na timu ya wataalamu wa Wizara ya Fedha na Mipango ya Tanzania kwa lengo la kupitia maeneo yote yaliyoanishwa katika matazamio ya ukuaji uchumi ya IMF na yale ya Serikali ya Tanzania.

"Mimi na Rais Magufuli tumekubaliana kuwa IMF na Tanzania watabaki kuwa wadau wanaoaminiana, tunaona fursa nyingi na muhimu katika nchi hii ikiwamo mipango mizuri ambayo Rais Magufuli ameianzisha.

Katika wiki zijazo, tutaendelea na mazungumzo na kuendelea kufanya kazi kwa ukaribu na Serikali ya Tanzania na tutaleta timu ya wataalamu watakaokuja kujadiliana na Serikali ya Tanzania ili kutazama maeneo yote yaliyofanyiwa mageuzi makubwa na kuyawianisha na ukuaji wa uchumi" alisema Selassie.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, aliwahakikishia Watanzania kuwa wizara yake imejipanga kutoa ufafanuzi wa maeneo yote ambayo yanapaswa kuwamo katika taarifa ya IMF ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania ikiwamo utekelezaji wa miradi mikubwa ya kiuchumi.

"Ili uchumi wa nchi ukue ni lazima uwe unawekeza, na bahati nzuri sana Rais amemueleza mgeni wake jinsi tunavyowekeza kwenye miundombinu hususani ujenzi wa reli ya kati, jinsi tunavyowekeza katika ujenzi wa bwawa kubwa litakalotupatia megawati 2,100 za umeme na pia miradi ya barabara

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

# Mdude wa Chadema aibua balaa bungeni

Na Sanula Athanas, DODOMA

MADAI ya kutekwa kwa kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Nyagali Mdude, maarufu Mdude Chadema', limetua bungeni.

Mbunge wa Iringa Mjini, Mch. Peter Msigwa (Chadema), ndiye aliyelipeka suala hilo bungeni jana, alipoalipoisimama na kutoa hoja ya dharura kwamba bunge kisitishe shughuli zake na kulijadili jambo hilo kwa dharura.

Hata hivyo, uamuzi wa Mch. Msigwa kulipeleka suala hilo bungeni uligeuka shubiri kwake kutokana na serikali kuliagiza Jeshi la Polisi limhoji kuhusu kutoonekana kwa Mdude.

Agizo la Mch. Msigwa kuhojiwa na Jeshi la Polisi lilitolewa na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Yusuf Masauni, alipopewa nafasi ya kutoa taarifa ya serikali bungeni juu ya kile kinachodaiwa kutekwa kwa Mdude.

Kada huyo wa Chadema anadaiwa kutekwa ofisini katika Mji wa Vwawa, Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe mwishoni mwa wiki.

Awali, baada ya kupewa nafasi na Mwenyekiti wa Bunge, Andrew Chenge, Mch. Msigwa alisimama na kusema: "Asante Mheshimiwa Mwenyekiti! Hivi karibuni katika nchi yetu kumekuwa na matukio ya mauaji, utekaji na watu kupotea.

"Ninapozungumza, juzi kuna kijana mmoja anaitwa Mdude Nyagali kule Mbozi ametekwa akiwa nyumbani kwake mbele ya macho ya watu, alipojaribu kupiga kelele, wale watu walionyesha silaha wakamkamata wakamweka kwenye buti ya gari.

"Tumekwenda kwenye vituo vya polisi, polisi wamesema siyo wao lakini wamekataa kufungua jalada. Mheshimiwa Mwenyekiti, haya matukio ambayo ukiangalia huku nyuma watu wengi ambao tuliwajadili hata kwenye hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani tulitaka serikali 'iji-commit'.

Kutokana na maelezo hayo ya Mch. Msigwa, Chenge aliipa serikali nafasi ya kutoa taarifa kuhusu tukio hilo au iliahidi Bunge kulipa taarifa hiyo baadaye.

"Ni kweli hili suala... suala lolote linalohusu maisha ya binadamu, ya Mtanzania, ni suala kubwa sana, lakini hiyo haimaanishi kwamba mtu anapotoweka... mimi hapa nina taarifa jimboni kwangu kuna kijana mmoja aliondoka nyumbani kwake tu hajaonekana mpaka leo.

"Sasa haiwezekani mtu ameamua tu kwenda kwa shughuli zake halafu hakurejea, ngoja, sikia nafika huko... mbona mna mambo ya... (kukawa na kelele kwenye Kambi ya Upinzani) najaribu kuwasaidia.

"Sasa tuwe tunatofautisha sana, lakini katika hili umesema na wananchi wameona na jitihada zikafanyika lakini bado maelezo yake si... hayajanyooka vizuri, mimi nadhani ingekuwa vizuri badala ya sisi kuanzisha mjadala ambao maudhui yake hatujafahamu sana kama wabunge, ni vema tu serikali ikatoa maelezo kama wanaweza sasa hivi lakini kama hawezi 'waji-commit' baadaye watoe maelezo ili Watanzania wajue kuhusiana na hali ilivyo," Chenge aliagiza.

Kutokana na agizo hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Ajira, Kazi, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisimama na kusema:

"Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ninaomba uridhie angalau kwa hatua ya awali kwa sababu wakati mwingine yanapotokea mambo kama hayo na serikali ikakaa kimya, sidhani kama tunajitendea haki pia sisi serikali na wananchi kwa ujumla.

"Kwa hiyo, kwa hatua hiyo ya mwanzo, ukiruhusu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani aweze kusema kitu kama anacho chochote cha kusema kwa hatua hii ya awali na aweze kuisemea serikali."

Baada ya kuruhusiwa, Masauni alisema: "Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kuonyesha masikitiko ya serikali kutokana na matukio machache ambayo yamekuwa yakijitokeza ya uhalifu nchini.

"Lakini kuhusiana na hoja hii mahsusi ambayo Mheshimiwa Msigwa amezungumza, kwa

INAENDELEA UK 5




## Rostam aomboleza kifo cha Mengi

Nimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha kaka yangu, mzee wetu, rafiki, kiongozi na mfanyabiashara wa miaka mingi, **Reginald Abraham Mengi.**

**Reginald Mengi** ameondoka akiacha nyuma yake urithi mkubwa wa uzoefu, ujuzi, mafanikio, kujifunza, kujisahihisha na kujitolea

Kupitia kwake, Mengi atabakia kuwa Mtanzania aliyeonyesha kwa vitendo kuwa mafanikio ni tunda la jitihada zinazotokana na ari na dhamira ya dhati ya mwanadamu kufanikiwa.

Kwa niaba yangu binafsi na ya familia yangu, napenda kutuma salamu za pole kwa mke, watoto, wanafamilia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote ambao wameguswa na msiba huu mzito.

**Rostam Azizi**
**Dar es Salaam**
**Mei 6, 2019**

## Waislamu leo kuanza mfungo Ramadhani

**Na Mary Geofrey**

WAUMINI wa dini ya kiislam, leo wanaanza mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na Kadhi Mkuu wa Tanzania, Abdallah Mnyasi, amethibitisha.

Akizungumza kupitia televisheni, wakati akifafanua kuhusu mwandamo wa mwezi, alisema juzi mwezi haukuonekana.


Alisema Waislamu ambao walitarajia kuanza kufunga jana, lakini hawakufanya hivyo kwa sababu mwezi haukuandama kama walivyotarajia. Alisema Waislam kote nchini wataanza mfungo wa Ramadhani mara baada ya kukamilika siku 30 za mwezi Shaaban.

Naye Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, alisema kwa kushirikiana na Mufti wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaabi na wa Tanzania Bara, Abubakar Zuber, wamekubaliana mwezi haujaonekana ila wataanza kufunga leo.

Alisema kwa maana hiyo mfungo huo utaanza rasmi leo na kuwataka Waislam wote kutumia mwezi huo kwa ajili ya toba na kutenda mema yanayompendeza Mwenyezi Mungu.

Ramadhan huanza mwezi wa tisa wa kalenda ya Kiislam ambapo Waislam wanaamini Kuran takatifu iliwasilishwa kwa Mtume Mohammad katika karne ya saba mnamo mwezi wa Ramadhan. Waislamu wanaamini kuwa huu ni mwezi wa kupatiwa msamaha na Mwenyenzi Mungu kwa hiyo huzidisha ibada kwa wingi na kuwa karibu na Mwenyenzi Mungu.

Ni mwezi wa toba, ambapo inatarajiwa waumini wa dini hiyo, watautumia kwa ajili ya kufanya ibada sana, lakini pia kutekeleza nguzo ya nne kati ya nguzo tano za dini hiyo, inayomtaka kila Muislamu mwenye afya njema, kufunga mwezi huu mtukufu unaoheshimika duniani kote.



Rais John Pombe Magufuli, akiwa katika mazungumzo na Mkurugenzi wa Idara ya Afrika wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Abebe Aemro Selassie, alipokutana naye Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU PICHA:**

## Mkenya matatani kisa kilo 15.8 heroin

**Na Hellen Mwango**

RAIA wa Kenya, Lucy Oding (39), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam akikabiliwa na tuhuma za kukutwa na dawa za kulevya aina ya heroine kilo 15.8.

Mshtakiwa alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mawakili wa Serikali, Constantine Kakula na Batilda Mushi, ulidai kuwa mshtakiwa anakabiliwa na shtaka moja.

Kakula alidai kuwa Aprili 21, mwaka huu mtaa wa Msimbazi, Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alikutwa akisafirisha dawa za kulevya kilo 15.8 aina ya heroine.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, uliomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

# Wabunge wataka tume ubadhirifu miradi ya maji

**Na Sanula Athaas,**
DODOMA

BAADHI ya wabunge wameltaka Bunge kuunda tume kuchunguza miradi yote ya maji nchini, wakieleza kuwa mingi imekwama au kutekelezwa chini ya kiwango kutokana na ubadhirifu.

Walitoa rai hiyo jana bungeni jijini Dodoma wakati wa mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka ujao wa fedha.

Mbunge wa Kibamba, John Mnyika (Chadema), alisema mwaka jana, serikali ilisema imeunda kamati iliyoongozwa na Prof. Tolly Mbwete, lakini hadi wakati anachangia, hakuna taarifa yoyote iliyotolewa juu ya jambo hilo.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, niliombe Bunge lako tukufu tukubali kuunda kamati ya kuchunguza udharifu pamoja na miradi kadhaa iliyojengwa lakini haitoi maji," Mnyika alishauri.

Vilevile, Mnyika, alisema hakubaliani na takwimu zilizotolewa na wizara kuhusu upatikanaji wa maji nchini, akieleza kuwa si za kweli.

"Serikali inaposema wananchi wa vijijini wanapata maji kwa asilimia 65 na mijini asilimia 80, takwimu hizi sio halisia. Hotuba ya upinzani ni ushahidi tosha wa upatikanaji wa maji nchini.

"Kwa hiyo, takwimu zilizotolewa na serikali si uhalisia, lakini hii inaonyesha serikali haijaamua kuweka kipaumbele kwenye suala la maji kama ilivyoamua kuwekeza kwenye kununua ndege.

"Tunaitwisha mzigo hii wizara bila sababu, tatizo serikali ndiyo haitoi fedha hata zile ilizoahidi, maji yanapaswa kupewa kipaumbele kwa sababu yanaongeza uzalishaji katika uchumi," Mnyika alisema.

Hoja ya kuundwa kamati ya tume kuchunguza miradi ya maji, pia ilizungumzwa na Mbunge wa Mbulu, Flatei Massay (CCM), aliyeiomba serikali kuunda tume kuchunguza miradi ambayo alisema imeshindwa kutekelezwa kwa muda mrefu.

Mbali na hilo, Massay alisema kuna tatizo kubwa kwa makandarasi kutolipwa fedha zao na kusababisha baadhi yao kuondoka kabisa kwenye maeneo ya miradi.

Mbunge wa Viti Maalum, Jaquline Msongozi (CCM), pia aliunga mkono hoja hiyo, akimtaka Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, kuliambia Bunge hatua zilizochukuliwa dhidi ya wabadhirifu wa miradi ya maji ambao wamesababisha miradi mingi kutokukamilika na kusababisha baadhi ya ndoa kuvunjika na wanawake kubaki wapweke.

"Mimi naomba sana wabunge tuongeze Sh. 50 ili iongezwe kwenye maji kwa sababu maji ndiyo maisha. Nakuomba sana Ustaadhi Prof. Mbarawa onyesha ujasiri wako tupate maji, naamini hii serikali sikivu ya Rais John Magufuli na haitatuangusha," alisema.

Naye Mbunge wa Urambo, Magreth Sitta (CCM), aliitaka serikali kueleza ni lini mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria utawafikia wananchi wa Mkoa wa Tabora hasa jimboni kwake ambako alieleza kuna changamoto kubwa katika upatikanaji wa maji.


TAARIFA KWA WATEJA WETU

USAJILI MPYA WA LAINI ZA SIMU

Ndugu Mteja, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano ya simu wanakutangazia kuwa, kuanzia Tarehe 1 MEI, 2019 watumiaji wote wa simu za mkononi ambao hawajasajili laini zao kwa kutumia mfumo wa alama za vidole wanatakiwa kusajili UPYA laini zao. Tembelea duka letu ukiwa na kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA kukamilisha usajili kwa mujibu wa sheria.

Imetolewa na:

ZANTEL smile TTCL airtel tigo halotel vodacom

Kwa kushirikiana na:

215214402

HABARI KITAIFA

# REGINALD MENGI Ninaringa kumwita rafiki

*ASUBUHI ya Mei 2, ilikuwa ni sikukuu nchini China na nilipanga kupumzika na kuitumia siku hiyo kusoma. Kwa bahati mbaya, mipango yangu ya kuwa na siku tulivu iliishia katika majanga majira ya saa nne asubuhi, pale nilipopata simu kutoka kwa Balozi Mwenzangu, Mheshimiwa Mbelwa Kairuki, Balozi wa Tanzania katika Jamhuri ya Watu wa China.*

*Kwa sauti ya utulivu, aliniuliza nilichokuwa nafanya na siku yangu ilivyoenda. Baada ya kuwa amesikia mwitikio wangu, alisema kwa sauti laini, kama vile kupunguza mshindo:"rafiki yako Reginald Mengi amefariki saa za mapema asubuhi huko Dubai".*

*Labda sehemu ya mshtuko kwa habari hizo ulikuwa ukweli kwamba sikuwa nimemuona Reginald, ambaye jamaa wa familia yangu humuita Bwana Mengi, kwa muda. Lakini tuliunganishwa miezi michache nyuma, na amekuwa akinisihi kumtembelea na kumpeleka mtoto wangu wa kiume ambaye alikuwa mtoto wake wa ubatizo kwa kuwa hajamuona kwa muda sasa. Tulikubaliana ziara hiyo ifanyike mwezi Desemba, na nilinunua hata tiketi zangu, lakini kwa sababu zisizojulikana, niliishia kutosafiri.*



Balozi wa Ghana katika Jamhuri ya Watu wa China, Edward Boateng.**PICHA: MTANDAO**

*Nilimjulisha ningekuja na familia yangu watoto wakirudi kwa ajili ya mapumziko. Labda hiyo ndiyo sehemu ya sababu, lakini nimejisikia kuguswa sana na kufariki kwa nguzo hii kuu ya biashara Afrika Mashariki na vyombo vya habari, taasisi ya Jumuiya Tanzania, mfadhili mkuu na kwa hakika mwanga ongozi wa ujasiriamli Afrika nzima.*

*Nilikutana kwa mara ya kwanza na Reginald, majira ya joto mwaka 1993 jijini London. Alikuja ofisini kwangu wakati huo nikifanya kazi na shirika la CNN. Alikuwa amepata maelekezo ya mawasiliano yangu kupitia kwa rafiki na alikuja kutafuta ushauri wa jinsi ya kuanzisha kampuni yake ya televisheni. Kutoka siku ya ziara hiyo, uhusiano wetu ulikua. Alikuja kuwa kaka yangu mkubwa, na familia yangu yote kutoka kwa baba na mama yangu, hadi kwa wakwe zangu wakaja kuwa familia yake katika pwani ya Afrika Magharibi. Siwezi nikaeleza jinsi walivyonyong'onywezwa na habari za kifo cha Reginald.*

*Tunathamini uzalendo wake, mapenzi kwa nchi na bara lake, familia na rafiki zake. Ni lazima nikiri nilivutiwa pia na hisia zake kwa matukio yasiyoisha ya "kijana wake mtukutu". Ninaweza kukumbuka nyakati nyingi za furaha tulizokuwa nazo pamoja iwe hapa Tanzania, Ghana, Afrika Kusini, London au Marekani na inavunja moyo nikimfikiria yeye kwamba hatakuwepo tena.*

*Kitu kimoja kilichonivutia kwake kilikuwa ni imani yake halisi ya kuwapatia Waafrika fursa. Nilisafiri naye maeneo mbalimbali duniani, tukakaa kwenye bodi tofauti ikiwamo meza ya kibiashara ya Afrika ambapo aliniteua mwaka 1994 kuchukua kiti chake wakati wa tukio moja la chakula cha mchana Arusha ambacho kiliniwezesha kukaa meza moja na Mwalimu Julius Nyerere. Hiyo kwa kweli ilikuwa siku nzuri kwangu na sijasahau kamwe mshangao huo.*

*Kitu kimoja muhimu nilichojifunza kutoka kwake ilikuwa ni imani yake kwamba haikuwa lazima kwa Waafrika matajiri kumiliki mali Ulaya au sehemu nyingine kuonyesha utajiri wao. Mara kwa mara aliniambia "Sitanunua kamwe mali nje ya Afrika. Kila makazi niliyonayo yako nchini Tanzania na hicho kinanifanya nijivune".*

*Alikuja kunitembelea Ghana wakati mtoto wangu wa kiume alipozaliwa, na kwa kweli wote waliokuwa kwenye karamu iliyoandaliwa kwa ajili yake walifurahi kwamba hadi leo hii, wanaendelea kuzungumzia msimamo wake na hisia zake za kindugu.*

*Aliamini katika nafasi na uwezo wa Mwafrika na alikuwa mmoja wa wadhamini wa kwanza na wafuasi wa Tuzo za Afrika za Waandishi wa Habari wa CNN ambapo nilianza kuwatambua waandishi magwiji wa Afrika wakati nikiwa na CNN. Ninakumbuka furaha yake kubwa na namna alivyocheza muziki usiku wote pale Betty Mkwasa alipokuwa Mtanzania wa kwanza kushinda tuzo hizo mwaka 2003.*

*Ninafaraijika kwamba aliongoza maisha kamili. Watanzania na Afrika mara kwa mara watakushukuru, Reginald kwa juhudi zako kubwa kutupeleka mbele. Rambirambi zangu za dhati kwa mkeo Jacqueline, Binti yako Regina, watoto wako wa kiume Abdiel, Jaden, Ryan na familia na taifa ulililoliacha nyuma.*

**Reginald, Ulale Mahali Pema Peponi, ulale katika amani ya kimbingu**

**Balozi. Edward Boateng**

**Balozi wa Ghana katika Jamhuri ya Watu wa China na Mwanzilishi wa Tuzo za Afrika za Waandishi wa Habari za CNN**

# Ushirikina wafunga zahanati

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, imeifunga zahanati ya kijiji cha King'ombe kutokana na watendaji wa zahanati hiyo kutishiwa na matukio ya kishirikina wawapo kazini.

Akizungumzia sababu za kufungwa kwa zahanati hiyo ofisini kwake jana, Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Jacob Mtalitinya, alisema halmashauri imeamua kuifunga zahanati hiyo mpaka hapo uongozi wa kijiji utakapokaa na wakazi wa kijiji hicho ili wakubali kuachana na vitendo hivyo.

Alisema zahanati hiyo ilifungwa zaidi ya mwezi mmoja uliopita, kutokana na watumishi wa afya waliokuwa wakifanya kazi katika zahanati hiyo kulalamikia kuwapo vitendo vya kishirikina.

"Nikweli tumeifunga zahanati hiyo kwa muda, mpaka hapo viongozi na wakazi wa kijiji hicho watakapokaa wakazungumza ili kukomesha vitendo hiyo... serikali haiamini masuala ya ushirikina, lakini kama vitendo vizuri vipo hata vibaya vipo pia, na hili ni suala la kiimani na tayari lilishajenga hofu kwa watendaji waliokuwapo," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema anasubiri taarifa ya kikao hicho na wakishakaa na kuonyana kuhusiana na tabia hizo, wakati wowote zahanati itafunguliwa, lakini ni vigumu kwa sasa watumishi kuendelea na kazi kwa kuwa wameingiwa na hofu.

Baadhi ya wahudumu wa afya waliliambia gazeti hili kuwa, watendaji walikuwa wakipigwa makofi na watu wasioonekana, kuanguka kifafa na wakati mwingine walikuwa wakikuta funza wamejaa katika vyumba vya kutolea huduma.

Kutokana na mazingira aiyo, walitoa taarifa kwa uongozi wa Manispaa ambao uliamua kuifunga kwa muda mpaka hapo wananchi watakapokutana na viongozi na kukemea vitendo vivyo.

Mtalitinya aliwasihi wakazi wa kijiji hicho kuwapa ushirikiano watumishi wa serikali waliopo katika kijiji hicho, na kama kuna tofauti ni afadhali wakatumie vikao kuziondoa kuliko kuwafanyia vitendo vya kishirikina.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Monica Peter, alisema hivi sasa wanalazimika kutembea umbali mrefu kwa kufuata huduma za afya.

# Mdude wa Chadema aibua balaa bungeni

INATOKA UK. 3

jambo hilo kuwa kuna kutekwa kwa kiasi.

"Mheshimiwa Mwenyekiti nataka nimsahihishe Mheshimiwa Mch. Msigwa si vizuri kumwita mbunge mwenzangu kuwa amezungumza uongo, lakini nimsahihishe na kwa taarifa alizozitoa, ambazo amezizungumza.

"Amesema kwamba huyo mtu ametekwa na vilevile polisi limekataa kutoa jalada kitu ambacho siyo sahihi, usahihi wa taarifa ni kama ifuatavyo -- ni kweli mtu huyu hakuonekana, na ukisema ametekwa maana yake wewe unajua.

"Sasa jambo la kwanza, kwa kuwa Mch. Msigwa amelithibitishia Bunge kwamba huyu mtu ametekwa, bila shaka yeye ana taarifa hizi. Kwa hiyo, niliekeze Jeshi la Polisi kwanza akalisaidie kabisa wamtafute, Mch. Msigwa alisaidie Jeshi la Polisi.

"Lakini pili, ni kwamba hapa sasa hivi tunapozungumza, Jeshi la Polisi limeshafungua jalada, si kweli kama ambavyo Mch. Msigwa anavyosema na uchunguzi umeshaanza na kwa kuwa suala hili tumelichukua kwa uzito, tumeongeza nguvu kutoka makao makuu kwenda kufanya uchunguzi huo.

"Lakini, kwa sababu jambo hili linataka kuchukuliwa kisiasa zaidi sasa Mheshimiwa Mwenyekiti na kwa sababu pengine limejitokeza kwa mwanachama wa chama fulani, maelekezo mengine ambayo tunataka tuyatoe ni kwamba tunaendelea kusisitiza wananchi kutoa nafasi kwa vyombo vya dola kufanya kazi yake.

"Kumekuwa kuna desturi ya baadhi ya wananchi hususani ni vijana kutumia mitandao ya kijamii vibaya kuichafua serikali, nataka nitoe wito kwa vijana hao kuwa waangalifu na Jeshi la Polisi liendelee vilevile kuwatafuta na kuwahoji wale wote ambao wanasambaza taarifa za kuchafua serikali kwenye mitandao ili na wenyewe wakaisaidie polisi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ukarabati wa shule za umma uungwe mkono

**MIONGONI** mwa sababu ambazo zimekuwa zikitajwa kuchangia kushuka kwa kiwango cha elimu nchini ni kukosekana kwa miundombinu rafiki katika shule zetu.

Hapa tunamaanisha uchakavu na uhaba wa majengo kama madarasa, mabweni, maktaba, ofisi za walimu na matundu ya vyoo. Hivi ndivyo ilivyokuwa kwa shule zetu nyingi za serikali.

Hali hii ilichangia kwa kiasi kikubwa mazingira ya wanafunzi kusomea na walimu kufundishia. Jibu la swali linaloweza kuulizwa ni kwamba ni kwa nini hali imekuwa hivi linaloweza kuwa ni kuwa hapakuwapo kipaumbele.

Hata hivyo, hali hiyo ni tofauti na miaka ya zamani ambapo elimu ilikuwa kipaumbele kikuu cha serikali kuanzia ukarabati, upangaji wa walimu wa kutosha katika shule pamoja na suala zima la ukaguzi wa shule.

Miaka ya baadaye kasi ya serikali ilishuka katika kusimamia na kuendesha shule zake na matokeo yake ni kuwa nyingi, hususan kongwe zikaporomoka kitaaluma (kufahaulisha), hivyo wazazi wengi hususan wenye uwezo kiuchumi kuanza kupeleka watoto wao katika shule za binafsi nje na ndani ya nchi.

Angalao baada ya serikali kuanzisha utaratibu wa kuzifanya baadhi ya shule zake kuwa za vipaji maalum katika miaka ya tisini, zilijaribu kubadili mtazano wa umma dhidi ya shule hizo, kutokana na kuongeza kiwango cha ufaulu. Hili linathibitishwa na matokeo ya shule hizo kama Mzumbe, Kibaha, Ilboru, Msalato, Kilakala, kwa kutaja baadhi kuwa mazuri na kushindana na shule bora za binafsi.

Serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani ilianzisha utaratibu wa kuzikarabati shule zake kwa lengo la kuboresha kiwango cha elimu. Kwa kuanzia ilianza kutenga bajeti na kuanza kukarabati baadhi ya shule hizo.

Juzi Serikali ilisema kwamba imetenga zaidi ya Sh. bilioni 257 kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe za Sekondari 89 nchini ambazo miundombinu yake ni chakavu.

Kwamba Lengo la hatua hiyo ni kuimarisha elimu na kuzifufua shule hizo ili ziweze kufanya vizuri kitaaluma kama ilivyokuwa zamani. Kati ya hizo katika mwaka wa fedha 2016/17 na 2017/18 tayari shule 46 zipo katika hatua mbalimbali za ukarabati wake.


Hayo yalibainishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, katika Kijiji cha Masanganya Kata ya Kibuta wilayani Kisarawe mkoani Pwani, alipokuwa akizindua madarasa mapya matatu na ukarabati wa madarasa mawili ujenzi uliofadhiliwa na Kampuni ya Yapi Merkez, inayojenga reli ya kisasa, ikiwa ni sehemu ya uwajibikaji na huduma kwa jamii.

Jafo alisema Rais John Magufuli ameamua shule zote zikarabatiwe ili kuleta tija ya elimu nchini, na kwamba hii inaonyesha ni kwa kiasi gani Serikali inataka elimu iende mbele zaidi kwa kuwa kwa sasa kila mwezi zinatengwa Sh.bilioni 23.85 kwa ajili ya elimu bure kwa watoto wote wa shule za msingi na sekondari.


Kutokana na umuhimu mkubwa wa miundombinu rafiki mashuleni, tunaishauri serikali kuhakikisha fedha zaidi zinatengwa kwa ajili ya ukarabati wa shule zake, ili kuwawekea wanafunzi na walimu mazingira rafiki ya kusomea na kufundishia.

Uamuzi wa serikali wa kuzikarabati shule ni wa kupongeza kwa kuwa ni chachu katika suala zima la kuboresha elimu. Hata hivyo, tunaelewa kuwa kazi ya ukarabati inahitaji fedha nyingi, lakini tunaamini inawezekana ikiwa utawekwa utaratibu mzuri na endelevu kwa kuishirikisha jamii na washirika wengine wa maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Raphael Kibiriti

# Mamlaka ziyamulike maduka yanayouza dawa za binadamu

**KUNA** Janga kubwa linaloendelea kuzinyemelea afya za Watanzania walio wengi nchini, kwamba lisipodhibitiwa sasa na mamlaka zenye dhamana linaweka rehani maisha yao.

Janga ninalolizungumzia linatokana na uwapo wa maduka holela ya kuuza dawa yaliyotapakaa karibu kila kona ya nchi ambayo baadhi yake hutoa huduma hiyo bila kuzingatia kanuni, maadili na taratibu za kitabibu zilizowekwa.

Kimsingi maduka yanayouza dawa za binadamu yanapatikana karibu kila kijiji, miji na majiji yakiwa katika ngazi tofauti tofauti.

Kwamba maduka haya ni afya za watu, ni uhai na ustawi wa taifa kwani ukizungumzia maduka ya kuuza dawa vijijini kwa mfano, unagusa asilimia 70 ya Watanzania, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

Muungwana anadiriki kusema kwamba baadhi ya maduka haya yamekuwa yakitenda kinyume cha sheria zilizoyaanzisha katika maeneo mengi.

Sababu kubwa ikiwa ni kujali fedha zaidi badala ya afya za watu na hivyo kukiuka taratibu na kanuni za kuanzishwa kwake.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kutambua umuhimu wa kushirikiana na sekta binafsi, iliruhusu kuanzishwa kwa maduka binafsi ya dawa katika dhima nzima ya kuboresha afya ya jamii.

Lakini mengi ya maduka haya yamekuwa hayaendi sambamba na sheria za uanzishwaji wake na hivyo kuipa kisogo dhima nzima hiyo ya serikali, inayolenga kuboresha afya ya jamii.

Sheria za uanzishwaji wa maduka haya zinataka mbali na usajili, ni lazima yawe na mtaalamu wa masuala ya famasia na yauze baadhi ya dawa za moto kwa kufuata maelekezo ya daktari yaliyoandikwa kwenye cheti cha mteja.

Hata hivyo, kumekuwa na malalamiko ya visa vya muda mrefu dhidi ya wafanyakazi katika maduka haya kutofuata sheria za kuanzishwa kwake, huku wananchi na wadau wa afya zao wakitaka mamlaka zichukue hatua zaidi.

Hatua kali zitakazosaidia kuzuia janga la kiafya linaloendelea kutengenezwa kwa makusudi na wamiliki ama wafanyakazi wa maduka haya.

Mojawapo ya visa vinavyotishia afya za Watanzania, kilitokea hivi karibuni jijini Dar es Salaam, ambapo mkazi mmoja aishie Tegeta alimpeleka mzazi wake mgonjwa katika zahanati moja ya serikali na kutibiwa.

Moja ya dawa alizoandikiwa na daktari haikuwapo katika zahanati hiyo na hivyo daktari akamshauri mkazi huyo akainunue kutoka maduka yanayouza dawa.

Mkazi huyo alienda katika duka moja la dawa akiwa na cheti cha daktari ambapo alipatiwa dawa na muuzaji kuwa ni dawa iliyoandikwa na daktari katika cheti alichokuwa nacho, na hivyo akaanza kumpatia mgonjwa wake.

Hata hivyo, baada ya siku nne kwisha bila hali ya mgonjwa kutengemaa, mkazi huyo alirudi kwa daktari ambapo daktari aliomba kuona dawa aliyokuwa akimpatia mgonjwa.

Kwa masikitiko makubwa daktari alikuta si ile aliyomwandikia mkazi katika cheti cha mgonjwa na akamshauri aende kwenye famasi yoyote kubwa katika eneo hilo la Tegeta, ambapo aliipata dawa halisi.

Dawa halisi iliyokuwa imeandikwa na daktari na kweli baada ya matumizi ya siku nne hali ya mgonjwa wake ilitengemaa.

Kuna mengi yanayoweza kuelezwa kutoka katika kisa hiki, lakini baadhi ni kuwa ama muuzaji katika duka hilo alijali pesa zaidi kuliko afya ya mgonjwa au hakuwa na taaluma ya famasia ambayo imeanishwa katika sheria, hivyo alishindwa kuelewa dawa iliyoandikwa na daktari.

Mojawapo ya mahitaji ya sheria ni kuwa na mwajiriwa aliye na utaalamu wa masuala ya famasia, kitu ambacho inawezekana hakifuatwi kwa mujibu wa kisa hiki.

Sasa kama hili lilitokea katika jiji la Dar es Salaam ambapo mamlaka zote zinazosimamia maduka haya zipo, vipi hali ilivyo vijijini?

Ni rai ya Muungwana kwa mamlaka zinazosimamia maduka haya zikachukua hatua sasa, vinginevyo kuna janga kubwa la kiafya linalowanyemelea Watanzania.

# Mapokezi ya Mwili wa Dk. Mengi pichani



Watoto wa Marehemu Dk. Reginald Mengi, Regina (wa pili kulia) na Abdiel (wa pili kushoto), wakiwa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Christopher Ole Sendeka (kulia) na Afisa Mwandamizi wa ITV/Radio One, Ayubu Semvua, baada ya mwili kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Umati wa waombolezaji wakiwa wamekusanyika katika makutano ya barabara za Uhuru na Kawawa, eneo la Ilala Boma, kwa ajili ya kumuaga marehemu Dk. Reginald Mengi. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda wakishiriki katika mapokezi ya mwili wa Dk. Reginald Mengi. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Mke wa marehemu, Jacqueline (katikati), baada ya kuwasili. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**



Baadhi ya watu wenye ulemavu wakilia kando ya barabara ya Kawawa eneo la Msimbazi Centre, wakati wakisubiri msafara wa gari lililobeba mwili wa marehemu. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Baadhi ya waombolezaji wakiwa na mabango yenye ujumbe mbalimbali kando ya Barabara ya Kawawa, eneo la Kinondoni. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Mapokezi ya kifalme

INATOKA UK 2

Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alilazimika kushuka kwenye gari lake ili kutoa maelekezo na baada ya hapo, wananchi walifungua njia na msafara kuendelea.

Wakati msafara huo ukitoka maeneo hayo, wananchi walianza kukimbia nao huku wengine wakitupia maua, nguo kama sehemu ya kumuenzi na kumuaga kipenzi chao Dk. Mengi.

Utupiaji wa maua kwenye gari lililobeba mwili wa marehemu ulifanyika tena eneo la Msimbazi Centre, lililopo Wilaya ya Ilala.

Msafara huo ulipofika maeneo ya Kigogo wananchi walishindwa kujizuia tena na kuamua kuuingilia, lakini baadaye waliuruhusu na ulipofika eneo la Magomeni Kanisani waombolezaji walijitokeza pande zote za barabara waliamua kulisukuma gari lilobeba mwili.

Msafara ulipofika eneo la Kinondoni Manyanya ulilazimika kupunguza mwendo na eneo la Ananasifu na Morocco msafara ulilazimika kusimama, huku wananchi wakionekana wakiwa juu ya daraja na wengine pande zote za barabara ili kumuaga Dk. Mengi.

Wakati msafara huo ulipofika Magomeni kuelekea Moroco, magari ya mwendokasi yalilazimika kusitisha safari zake kwa muda kutokana na wingi wa watu waliokuwa wakitumia njia za magari hayo.

Baadhi ya watu waliojitokeza kwenye msafara huo walisikika wakiimba kuwa ni halali kwa Watanzania walivyojitokeza kupokea na kuaga kwasababu Dk. Mengi ameisaidia Tanzania na Watanzania wengi.

Kutokana na idadi kubwa ya watu, baadhi ya wananchi walizimia na kuchukuliwa na gari kubeba wagonjwa lililokuwa kwenye msafara huo na kuwahishwa hospitali.

MVUA YAANZA

Msafara ulipofika eneo la Morocco ulikutana na mvua kubwa, lakini hali hiyo haikuwafanya wananchi kuacha kusimama barabarani kumsubiri mpendwa wao ili wamuage.

Waendesha bodaboda walionekana kuongezeka kadri msafara huo ulipokuwa ukiendelea na ulipofika eneo la Victoria, ulisimama kwa muda ili kutoa fursa kwa kundi kubwa la wananchi lililokuwa eneo hilo kutoa heshima kwa Dk. Mengi.

Licha ya msafara huo kuongeza mwendo, huku mvua ikiendelea kuongezeka, lakini wananchi walionekana wakikimbia nao huku wengine wakiwa wameshika majani na maua.

Msafara huo ulipofika maeneo ya Sayansi ulisimama kwa mara nyingine na katika hali ambayo haikutarajiwa baada ya kuwasili eneo la kituo cha ITV, ambacho kimebeba jina la Kituo chake cha Televisheni ITV, maelfu ya wananchi walifunga barabara kwa dakika zaidi ya kumi.

Baada ya kufika maeneo ya Mwenge sokoni, msafara huo ulilazimika kusimama kwa mara nyingine, huku wananchi wakiimba jimbo mbalimbali za kumsifu.

MABANGO YATAWALA

Maeneo mbalimbali ambako mwili huo ulipita baadhi ya wananchi waliokuwa wakiusubiri mwili huo wa Dk. Mengi walibeba mabango yenye jumbe mbalimbali za kumsifu na kumshukuru kwa mema aliyoyatenda.

"Asante Mengi kwa ajira, kwa kuondoa umaskini na kukuza uchumi wa nchi, R.I.P Mengi"

Bango lingine lilisomeka, "Dk. Mengi, Never Before and Never Again"

"Dk. Mengi tutakukumbuka daima, I Can, I Must, I Will"

**Imeandaliwa na Romana Mallya na Elizabert Zaya**



Meneja wa Kitengo cha Damu Salama Mkoa wa Dodoma, Dk. Leah Kitudya (L) akimtoa damu mmoja wa wakazi wa jiji hilo, aliyefika kuchangia damu katika maadhimisho ya Wiki ya Wanasayansi wa Maabara za Afya Tanzania, yanayoendelea katika viwanja vya Nyerere Square, jijini humo jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPHI**.

## ...Mwinyi: Kifo chake pigo kwangu, maelfu kwenda Hai

INATOKA UK 2

Kampuni ya ukandarasi ya Kalsi & Jutley Ents Ltd ya Moshi ndiyo iliyopewa zabuni ya ujenzi na upambaji wa kaburi ambalo atazikwa Dk. Mengi, baada ya uchimbaji wa asili kufanywa na majirani wa marehemu.

Kiongozi wa itifaki nyumbani kwa Dk. Mengi huko Kisereni, Wilfred Mushi amethibitisha kuwa waliopewa kazi ya ujenzi wa nyumba ya milele ya Mwenyekiti Mtendaji wa IPP ni Kampuni ya ukandarasi ya Kalsi & Jutley Ents Ltd.

Kaburi la Dk. Mengi ambalo atazikwa, limechimbwa sentimeta chache kutoka alikozikwa mwanae, Rodney Mutie Mengi, ambaye alizikwa katika makaburi ya familia ya Dk. Mengi Oktoba 6, 2005.

**Imeandikwa na Romana Mallya (Dar) Godfrey Mushi (HAI)**

## JPM, kigogo wa IMF wateta Dar

INATOKA UK. 2

na viwanda vingi vilivyojengwa, haya ndio yanayokuza uchumi na sisi tunaamini kabisa wenzetu hawakuyazingatia kabisa katika taarifa ya awali (iliyovuja)" alisema Dk. Mpango.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, aliwatoa shaka wawekezaji kutoka nchi mbalimbali kuendelea kuwa na imani na mazingira ya uwekezaji ya Tanzania na amewataka Watanzania kutokua na hofu kwamba wawekezaji watapungua kwani wawekezaji hao wanaendelea kuja.

"Nashukuru kwamba hata wawekezaji wenyewe hawana hofu kwani hata baada ya taarifa hiyo kuwa imevujishwa bado wengi wameendelea kuja na kuonesha nia ya kufanya kazi na sisi, na nashukuru Shirika la Fedha la Kimataifa kwa kuja kuzungumza na sisi, hiyo ni dalili kuwa shirika hili bado lipo nasi na bado tunaendelea na mazungumzo, wale ambao walidhani pana ugomvi mkubwa kati ya IMF na Tanzania walikuwa wamekosea kabisa, na msimamo wa Tanzania utafahamika baada ya mazungumzo kuanza na kuwapitisha katika miradi mikubwa ya maendeleo ambayo inafanyika" alisema Prof. Kabudi.




HABARI KITAIFA

## USAHIHI

Katika tangazo la Wizara ya Maji jana kwenye ukurasa huu, liliandikwa kwa makosa kwa kumuita Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, kuwa ni Naibu Waziri Mkuu - **Mhariri**

## Wakazi Ukara wapongeza kasi ya ujenzi wa kituo afya

**Na Rose Jacob,** UKARA

WAKAZI wa Kisiwa cha Ukara wilayani Ukerewe mkoani Mwanza, wamemshukuru Rais John Magufuli kwa ujenzi wa kituo cha Bwisya kinachojengwa kwa hadhi ya hospitali ya wilaya.

Ujenzi huo unafanywa na mkandarasi Suma JKT, kwa gharama ya zaidi ya Sh.milioni 800 zilizotokana na rambirambi ya ajali ya kuzama kivuko cha MV Nyerere Septemba mwaka jana.

Shukurani hizo zilitolewa kwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella (pichani chini), wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo, ambapo majengo ya wodi yalikuwa yamefikia asilimia 90, huku akiagiza ianze kutumika Mei, 30 mwaka huu.

Hata hivyo, pamoja na pongezi hizo, wananchi hao wameiomba serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya usafiri wa majini katika Ziwa Victoria kutoka Bugorora kwenda kwenye kisiwa cha Ukara.

Akizungumza na wananchi hao katika eneo la kituo cha afya Bwisya, Mongella alisema serikali inatarajia kukamilisha ujenzi wa kituo hicho na kuanza kutumika ndani ya mwezi mmoja ili kuhakikisha wananchi wa kisiwa hicho wanaondokana na adha ya upungufu wa vyumba vya kulazwa wagonjwa.

"Ifikapo Mei mwaka huu, majengo haya yataanza kutumika na wananchi wasiwe na hofu ya kupata huduma bora, maana serikali inaongeza watumishi katika kituo hiki...dawa zipo za kutosha, hivyo hakuna haja ya kushindwa kufika kupata huduma za matibabu kwa kuwa serikali ya Rais Magufuli inataka kuona wananchi wake wanakuwa na afya njema," alisema Mongella.

Aidha, Mongella aliwataka watumishi katika kituo hicho kutoa huduma kwa kufuata maadili na taratibu za kazi badala ya kuwahangaisha wagonjwa kwa kushindwa kuwapatia majibu kwa wakati mwafaka ili kuepuka kuwapotezea muda na kujikuta ungonjwa umeshawaathiri.



# Bilioni 257/- kukarabati shule kongwe nchini

**Na Grace Semfuko,** MAELEZO

SERIKALI imetenga zaidi ya Sh. bilioni 257 kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe za Sekondari 89 nchini ambazo miundombinu yake ni chakavu.

Lengo la hatua hiyo ni kuimarisha elimu na kufufua shule hizo ili ziweze kufanya vizuri kitaaluma kama ilivyokuwa zamani.

Kati ya hizo katika mwaka wa fedha 2016/17 na 2017/18 tayari shule 46 zipo katika hatua mbalimbali za ukarabati wake.

**Kati ya hizo katika mwaka wa fedha 2016/17 na 2017/18 tayari shule 46 zipo katika hatua mbalimbali za ukarabati wake.**

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, katika Kijiji cha Masanganya Kata ya Kibuta wilayani Kisarawe mkoani Pwani wakati akizindua madarasa mapya mitatu na ukarabati wa madarasa mawili, ujenzi uliofadhiliwa na Kampuni ya Yapi Merkez inayojenga reli ya kisasa, ikiwa ni sehemu ya uwajibikaji na huduma kwa jamii.

"Mheshimiwa Rais ameamua shule hizi zote zikarabatiwe ili kuleta tija ya elimu nchini...hii inaonyesha ni kwa kiasi gani Serikali yetu inataka elimu iende mbele zaidi kwani tunashuhudia hivi sasa kila mwezi Sh. bilioni 23.85 zimetengwa kila mwezi kwa ajili ya elimu bure kwa watoto wetu, ndugu zangu hili sio jambo dogo," alisema Jafo.

Aidha, alibainisha kuwa Wilaya ya Kisarawe imeanza mchakato wa ujenzi wa shule ya kwanza kidato cha tano na sita maalum kwa ajili ya wasichana katika Kata ya Kibuta lengo likiwa ni kuinua kiwango cha elimu ya mtoto wa kike.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, alisema mkoa huo sasa unafanya vizuri kwenye elimu kwani ufaulu wa darasa la saba kwa mwaka 2017 ulishika nafasi ya 19 kati ya 26 kitaifa, nafasi ambayo imepanda kwa mwaka 2018 na kufikia ya 11 kati ya 26 hivyo kuwataka wadau wa elimu kuzidisha jitihada za ufundishaji na uboreshaji wa miundombinu ya elimu mkoani humo.

Nae Kaimu Afisa Uhusiano wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Jamila Mbarouk, alisema shirika kwa kushirikiana na Yapi Merkez inayojenga reli ya kisasa, wameamua kujenga madarasa mapya matatu na kukarabati mawili kutokana na kuona umuhimu wa sekta ya elimu nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, alisema wilaya yake imekuwa ikifanya vizuri kwenye elimu ambapo mwaka 2016 ilifaulisha wanafunzi kwa asilimia 67.6 kiwango ambacho kilipanda kwa mwaka 2018 na kufikia 67.6, huku shule ya Masanganya iliyofadhiliwa ujenzi wake ikishika nafasi ya nane kati ya shule 58 zilizopo kwenye wilaya hiyo.



Mwendesha bodaboda akiwa amepakia abiria na mzigo katika barabara ya Morogoro, eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# UDSM yajivunia utafiti kubadili sera

**Na Mary Geofrey**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kimesema kimekuwa kikifanya utafiti unaogusa maisha ya wananchi wa kawaida wakiwamo wakulima na tatizo la ajira ambazo hutumika kubadilisha sera za nchi.

Hayo yameelezwa na Naibu Makamu Mkuu wa UDSM, Dk. Ambrose Itika, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu wiki ya tano ya utafiti iliyoanza hadi Jumatano.

Alisema utafiti mbalimbali unaofanywa na chuo hicho, umekuwa zikitoa na ufumbuzi wa changamoto zinawagusa wananchi moja kwa moja.

"Tumekuwa tukifanya utafiti mara kwa mara na umekuwa ukiwagusa wananchi wa kawaida moja kwa moja kwa sababu tunafanya katika maisha ya kawaida ya wananchi hasa vijiji kuhusu kilimo, lakini pia kuhusu suala la ajira na hatuishii hapo tunaeleza pia suluhisho la changamoto hizo," alisema Dk. Itika.

Alitawaka wananchi wa kawaida kushiriki katika wiki hiyo ili kujifunza mambo mbalimbali ya utafiti na namna ambavyo wananufaika nao bila wao kufahamu.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Uafiti na Machapisho, Prof. Dev Jani, alisema mada ya kongamano hilo ni 'Utafiti kwa Maendeleo Jumuishi na Endelevu'.

Alisema chuo hicho kinatumia fursa hiyo kujipambanua katika utafiti, uvumbuzi, huduma kwa jamii na ubadilishaji maarifa katika kutatua changamoto mbalimbali za kijamii nchini.

Alisema pia kutakuwa na kongamano litakalowashirikisha wanajopo nguli kutoka katika mashirika ya umma, binafsi, kimataifa na taasisi za kitaaluma watakaojadiliana kuhusu mada kuu na kutoa mapendekezo mahusus ya mustakabali wa maendeleo endelevu nchini.

# 4,000 waliotumbuliwa vyeti feki warejeshwa

BUNGE limeelezwa kuwa watumishi 4,160 walioondolewa wakati wa uhakiki wa vyeti feki vya kitaaluma na kitaalamu wamebainika kuondolewa kazini kimakosa au kwa uonevu na wamerejeshwa kazini.

Kati ya watumishi hao waliorejeshwa kazini, 3,057 ni watendaji wa vijiji, mtaa na kata.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, aliyasema hayo bungeni jijini Dodoma jana alipojibu swali la Mbunge wa Musoma Mjini, Vedastus Manyinyi (CCM).

Mbunge huyo alisema serikali katika kuhakikisha inapata watumishi bora wenye sifa, iliamua kuwaondoa kwenye utumishi watumishi wasio na sifa pamoja na wenye vyeti feki.

"Je, kwanini serikali isiunde timu maalum ili ipitie kila halmashauri kupitia taarifa juu ya zoezi hilo ili haki itendeke hasa kwa wale ambao hawana uwezo wa kwenda wizarani?" mbunge huyo alihoji.

**Je, kwanini serikali isiunde timu maalum ili ipitie kila halmashauri kupitia taarifa juu ya zoezi hilo ili haki itendeke hasa kwa wale ambao hawana uwezo wa kwenda wizarani?**

Alisema wapo watumishi waliojiendeleza kielimu lakini wameondolewa kwa kosa la udanganyifu.

"Je, serikali haioni kuwa hao ni bora kuliko wale ambao hawajajiendeleza?"mbunge huyo alihoji.

Akijibu maswali hayo, Mwanjelwa alisema katika uhakiki watumishi 15,189 walibainika kuwa na vyeti vya kughushi na kuondolewa kwenye orodha ya malipo ya mshahara.

Hata hivyo, kiongozi huyo wa serikali alisema baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa watumishi na vyanzo vingine kuhusu watumishi kuondolewa kimakosa au kwa uonevu katika orodha ya mishahara, serikali imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa karibu ikiwa ni pamoja na kuunda timu za ufuatiliaji wa utekelezaji wa uhakiki huo.

Alisema kwa upande wa watumishi wanaojiendeleza kielimu kutoka elimu ya darasa la saba, wanafanya vizuri na serikali inahimiza watumishi kujiendeleza kielimu.

Alisema kwa mujibu wa Kanuni D.12 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2009, ni makosa kwa mtumishi kujipatia ajira kwa njia ya udanganyifu.

"Hivyo serikali ilielekeza waajiri kuwaondoa kwenye orodha ya mishahara watumishi wa umma walioajiriwa kabla ya Mei 20, mwaka 2004, ambao katika kumbukumbu zao rasmi za kiutumishi, walijaza taarifa za udanganyifu kuwa walifaulu mitihani ya kidato cha nne lakini hawakuthibitisha taarifa zao kwa kuwasilisha vielelezo vya sifa hizo," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji lini serikali itaunda tume ya kuzunguka kwenye halmashauri ili wale ambao hawakupata nafasi ya kufika ofisi ya utumishi warudi kazini.

"Serikali ina mpango gani wa kuwapa kifuta machozi walioondolewa ambao walikuwa wamebakisha mwaka mmoja kazini," mbunge huyo alihoji.

Katika majibu yake, Mwanjelwa alisema serikali ilishafanya ufuatiliaji kwa asilimia 95 na watumishi walioandika taarifa za uongo hawataruhusiwa kuwa watumishi wa umma.



Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai (kulia), akimsikiliza Kaimu Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Natalie Bovely, alipomtembelea ofisini kwake, jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Ajali barabarani sasa zapungua




SERIKALI imesema mkakati maalum wa kupunguza ajali za barabarani umefanikiwa kuzipunguza kwa asilimia 43 mpaka sasa.

Imeelezwa kuwa mkakati huo ulihusisha mbinu mbalimbali zenye lengo la kuwalazimisha madereva kufuata sheria za usalama barabarani.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Maryam Salum Msabaha (Chademna). Mbunge huyo alisema kumekuwa na baadhi ya askari barabarani wanaosimamisha magari hasa yale ya safari ndefu wakitokea vichakani na wakati mwingine askari hao kusababisha ajali.

"Je, ni askari wangapi wenye tabia hizi na kama wameshachukuliwa hatua za kinidhamu?" mbunge huyo alihoji.

Katika majibu yake, Masauni alisema wakati serikali ya awamu ya tano inaingia madarakani, kulikuwa na mfululizo wa ajali nyingi za barabarani husussan zile zinazohusisha magari ya abiria.

Alisema kwa kuzingatia hilo, Baraza la Usalama wa Barabarani lilibuni mkakati maalum uliofanikiwa kupunguza ajali kwa asilimia 43 mpaka sasa na mkakati huo ulihusisha mbinu mbalimbali.

Hata hivyo, alisema serikali haina ushahidi wa matukio ya askari waliowahi kusababisha ajali barabarani kutokana na kujificha vichakani. Alisema serikali kupitia Baraza la Taifa la Usalama Barabarani limejiwekea utaratibu wa kufanya uchunguzi wa kina kwa kila ajali kubwa inayotokea na kuchukua hatua stahiki inapobainika kuna uzembe wa usimamizi wa sheria au uvunjifu wa sheria za usalama barabarani.

"Jeshi la Polisi chini ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168, linamtaka askari polisi kuhakikisha usalama wa watumiaji wote wa barabara," alisema.

Naibu waziri huyo aliongeza kuwa katika kutekeleza majukumu yao hayo, polisi wanatumia mbinu kwa mujibu wa sheria na taratibu zinazowaongoza.

Katika swali la nyongeza , mbunge huyo alisema askari wamekuwa na matukio ya kujificha kichochoroni na wanaposimamisha gari wanasimamisha ghafla na kuhoji mkakati wa serikali kudhibiti tabia ya kujificha vichochoroni.

## Fidia kwa waliolipisha Mchuchuma zachakatwa

WIZARA ya Viwanda na Biashara imesema mchakato wa malipo ya fidia kwa wananchi walioachia maeneo yao kupisha miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na Liganga unaendelea.

Imesema fidia hiyo italipwa baada ya uthaminishaji na pindi taratibu za msingi za kimaandalizi zikikamilishwa.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Ludewa, Deogratias Ngalawa (CCM).

Katika swali lake, mbunge huyo alisema serikali iliahidi kuwalipa fidia wananchi waliaoachia maeneo yao kupisha miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na Liganga, lakini mpaka sasa hawajalipwa.

"Je, lini serikali italipa fidia wananchi waendelee na shughuli nyingine za kiuchumi? Kwanini serikali haitoi mrejesho pindi panapotokea mkwamo, Pia, serikali inaweza kuthibitisha kuwa miradi hii itaanza kutekelezwa mwaka 2017 kama ilivyoahidi bungeni?" mbunge huyo alihoji.

Katika majibu yake, Manyanya alisema kazi ya uthaminishaji mali za wananchi watakaopisha mradi unganishi wa Mchuchuma na Liganga awamu ya kwanza ilikamilika Agosti 18, 2015.

Alisema ulipaji wa fidia kwa wakati huo haukufanywa kwa kuwa muda mrefu ulikuwa umepita, hivyo serikali ilifanya uhakiki wa uthaminishaji mwingine Desemba mwaka jana na imebainisha malipo stahiki yatakayopaswa kulipwa.

"Taratibu hizi zimekuwa shirikishi na zikifanywa kwa kuwahusisha mamlaka husika ikiwamo mamlaka ya serikali za mitaa katika maeneo ya miradi.

"Malipo ya fidia kwa mujibu wa uthaminishaji wa sasa utafanywa pindi taratibu za msingi za maandalizi zikikamilishwa na serikali," alisema.

Aliongeza kuwa mradi huo umeanza kutekelezwa kwa kufanya maandalizi ya awali ambayo pamoja na mambo mengine yanayojumuisha upambuzi yakinifu wa mradi, uthaminishaji wa mali na maeneo ya wananchi watakaopisha mradi na kujenga barabara ya kiwango cha changarawe.

Alifafanua kuwa barabara hiyo itaunganisha eneo la mradi na barabara kuu ya lami ili kuwezesha kufikisha mitambo na huduma nyingine katika eneo la mradi.

Alisema pamoja na jitihada hizo, kasi ya utekelezaji imekuwa ndogo kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza hususani majadiliano na mwekezaji kuchukua muda mrefu zaidi kuliko ilivyotegemewa.



## HABARI ARUSHA

# Polisi wapigwa jeki ya matairi ya gari

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

JESHI la Polisi Mkoa wa Manyara, limepatiwa msaada wa matairi manne ya gari na mdau wa maendeleo mkoani humo, Toima Kiroya, ili kuhakikisha ulinzi kwa raia na mali zao unakuwa vizuri wakati wote.

Msaada huo aliutoa hivi karibuni mjini hapa na kuukabidhi kwa Mkuu wa Mkoa huo, Alexander Mnyeti, ili aupokee kwa niaba ya Rais na wananchi.

Toima alisema anaamini msaada huo utalisaidia Jeshi la Polisi, kupunguza adha ya usafiri ambayo pengine ilikuwa inawakabili.

"Uliponishirikisha kwenye hili sikusita kusaidia kama mdau wa maendeleo, kwa hiyo tutaendelea kusaidia kuleta maendeleo na kufanya hivi ni uzalendo wa hali ya juu...mimi kama Mtanzania wa kawaida,"alisema Toima.

Alisema ameamua kusaidia juhudi za serikali kwa kuwa ndio imemsomesha bure, na amefanya kazi nyingi za serikali na nguvu bado anazo, hivyo anaona anastahili kuendelea kutumika kupitia kuunga mkono jitihada zinazoendelea.

Mnyeti alimshukuru mdau huyo wa maendeleo kwa kusaidia upatikanaji wa matairi hayo yenye thamani ya Sh. milioni 1.2, na akamtaka kutosikiliza maneno ya watu wanaompiga vita anapojenga mbindombinu ya huduma za kijamii.

Mnyeti alisema Toima amewajengea shule watu wa Wilaya ya Simanjiro na sasa anajenga chuo cha ufundi stadi, ingawa kuna watu wanampiga vita, alimshauri asiogope bali aendelee hivyo asiwasikilize wanaomkatisha tamaa.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Augustino Senga (pichani chini), alimshukuru mdau huyo kwa msaada huo, huku akisema hali ya magari yao haikuwa ya kuridhisha, hivyo msaada huo umefika kwa muda mwafaka na alimpongeza kwa kuthamini kuwapo kwa amani.

Alifafanua kuwa serikali imekuwa ikiwasaidia, ila bado wana uhitaji, hivyo wakipatikana wadau wa kusaidia ni jambo jema, kwa ajili ya kuimarisha usalama wa raia na mali zao.




# RPC Shana awafunda waandishi wa habari

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KAMANDA wa Polisi mkoani Arusha, Jonathan Shana, amewataka waandishi wa habari kufanya jitihada kuzifahamu sheria za uchaguzi na vyama vya siasa vizuri, ili waweze kuandika habari zao kwa usahihi katika kipindi cha uchaguzi ujao.

Akizungumza mwishoni mwa wiki jijini hapa na waandishi wa habari, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, Kamanda Shana alisema ni vema kila mwandishi wa habari akazifahamu vizuri sheria za uchaguzi na vyama vya siasa ili kuepuka kuandika habari ambazo zinakwenda kinyume cha misingi na maadili ya taaluma hiyo.

"Nyie ndio mmeshika kalamu ambazo ni silaha muhimu sana, mkitaka kuharibu amani mnaweza na kuilinda mnaweza, sasa kuelekea uchaguzi hakikisheni mnazifahamu sheria za uchaguzi ili muweze kutenda haki katika kalamu zenu, na mimi mwanasheria mkinitaka pia niwafundishe baadhi ya sheria niko tayari mnitumie," alisema.

**Nawaomba sana tushirikiane katika hili maana tatizo kubwa Arusha kuna kesi nyingi za watoto na wanawake kubakwa.**

Alisema kuwa Tanzania kuna uhuru, lakini hakuna uhuru usio na mipaka na kila mwanahabari anapaswa kufahamu hilo, ili aweze kujilinda na kujiepusha na masuala yasiofaa.

Kamanda Shana alisema kila mtu akiweka mbele uzalendo na kutafakari habari anayoandika kama ina maslahi mapana kwa nchi, itawezesha nchi kwenda salama na uchaguzi kupita salama.

Aidha, aliomba wanahabari kutumia kalamu zao kupigania haki za watoto na wanawake wanaobakwa na kesi zao kuishia kumalizwa kienyeji kupitia vikao vya ukoo.

"Nawaomba sana tushirikiane katika hili maana tatizo kubwa Arusha kuna kesi nyingi za watoto na wanawake kubakwa, lakini kesi hizi zinamalizwa katika vikao vya ukoo na tatizo linazidi kukua, tumieni kalamu zenu kupigania haki za makundi haya na kuwafichua wabakaji," alisema.

Pia alisema hata ndoa za jinsia moja sio za kushabikia kwa kuwa vitabu vya dini na mila na destruri za nchi haziruhusu, hivyo ni vema kalamu za wanahabari zikatumika kuelimisha wananchi wafahamu madhara yake.

Alimalizia kwa kusisitiza kila mwanahabari kujiepusha na kutumiwa na mtu yoyote na hasa wanasiasa ili kuharibu amani.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Arusha (APC), Claud Gwandu, alisema katika maadhimisho ya mwaka huu kwa mkoa huo, wametoa kipaumbele kwa kutoa elimu kwa wanahabari kufahamu masuala ya uchaguzi, ili kujiweka tayari katika kipindi kijacho cha chaguzi za serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani.



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, akikabidhi kitambulisho kwa mfanyabiashara mdogo katika Soko la Ngaramtoni, wilayani humo Mkoa wa Arusha. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Gambo, Muro washiriki kugawa vitambulisho

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo kwa kushirikiana na Mkuu Wilaya ya Arumeru, jana waligawa vitambulisho vya wajasiriamali awamu ya pili, ili kuhakikisha kila machinga anakipata.

Mkuu wa mkoa huyo pia alikabidhi Wilaya ya Arumeru vitambulisho hivyo 10,000 ambavyo vitagawiwa kwa halmashauri mbili zilizopo ndani ya wilaya hiyo.

Akizungumza kuhusiana na ugawaji huo Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro alisema hiyo ni awamu ya pili ya ugawaji wa vitambulisho na awamu ya kwanza waligawa, hivyo atahakikisha kila halmashauri inapata vitambulisho 5,000.

Alisema baada ya kuvipokea vitambulisho hivyo alivigawa katika soko la Tengeru, vitambulisho 1000 kwa wafanyabiashara na wataendelea kuvigawa hadi wafanyabiashara wote wavipate.

"Kama mnavyoona mimi na timu yangu yote tumeingia sokoni na tumefanyakazi mmeona watendaji wangu wa kata wafanyakazi wa halmashauri wote, bila kujali cheo tumeingia kugawa vitambulisho vya machinga na tumegawa vitambulisho 1,000 na tunaendelea kugawa katika masoko yote," alisema Muro.

Alimshukuru Mkuu wa Mkoa wa Arusha kwenda kuwapa ushirikiano katika zoezi hilo, kwani amewapa motisha ya kutosha.

Naye RC Gambo alisema ameamua kuwapa motisha ya ugawaji wa vitambulisho watumishi wa wilaya hiyo kwa kushirikiana nao katika zoezi la ugawaji na kuwataka kuendelea na hilo.



# Wadaiwa sugu wa bili maji kuburuzwa kortini

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MAMLAKA ya Bonde la Maji la Mto Pangani mkoani Kilimanjaro, inakusudia kuwafikisha mahakamani wadaiwa sugu wa bili za maji, pamoja wale waliochimba visima bila vibali vya mamlaka hiyo.

Mkurugenzi wa bonde la Pangani, Sengule Sengule, alisema kumekuwapo tatizo baadhi ya wateja wakubwa ambao ni makapuni na taasisi kukwepa kulipa bili za maji, huku wakiendelea kutumia maji.

Alisema kutokana na tatizo hilo mamlaka inakusudio la kuwafikisha mahakamani wadaiwa sugu wote kwa mujibu wa sheria.

**Kutokana na tatizo hilo mamlaka inakusudio la kuwafikisha mahakamani wadaiwa sugu wote kwa mujibu wa sheria.**

"Kuna baadhi ya wateja wetu wakubwa ambao ni kampuni na taasisi wamekuwa wakikwepa kulipa bili za maji kwa zaidi ya miaka mitano na kuendelea, na tumewafuatilia, lakini bado wamekaa kimya...sasa sisi kama mamlaka ambayo inawasimamia wateja hao tumefikia hatua za kufuata sheria," alisema Sengule.

"Sheria inaturuhusu sisi kama mamlaka kuwachukulia hatua za kisheria wadaiwa sugu wanaokataa kulipa bili, hivyo tumeamua kuchukua hatua ili walipe bili za maji kwa maslahi mapana ya nchi," alisema.

"Kwa sababu hizi sheria hatutungi sisi, imetungwa na bunge ambalo ni wawakilishi wa wananchi kwa maslahi mapana ya nchi, hivyo sisi kazi yetu ni kuzifuata sheria hizo," alisema.

Katika hatua nyingine, alisema bonde hilo pia limeanza zoezi la kuchunguza uchimbaji wa visimi katika maeneo mbalimbali na kwamba watakaobainika hawana vibali, watachukuliwa hatua za kisheria.

"Tupo kwenye zoezi la kuchunguza utoaji wa vibali vya uchimbaji wa visima na zoezi hili limeshaanza Tanga na baadae Kilimanjaro, ila nawaasa tu waliojichimbia visima bila kibali wafike kwenye ofisi za mamlaka wasisubiri adhabu," alisema.

Aidha, alisema kazi ya bonde ni kutoa vibali kwa watumia maji kwa kufuata sheria na kanuni za bonde pamoja na kutunza vyanzo vya maji, mito na mifereji yote.



Wachuuzi wa ndizi wakisaka wateja katika mitaa ya mji wa Babati, mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Tanzania yapewa 5 uzalishaji mchele bora

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TANZANIA imetajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazozalisha mchele mzuri na msafi na ambao una thamani ukilinganisha na mchele unaozalishwa Msumbiji, Kenya, Rwanda na Burundi.

Pia imetajwa nchi yenye idadi kubwa ya wanawake wanaozalisha kwa wingi zao hilo ambapo huzalisha tani 5-8 kwa hekta.

Hayo yalibainishwa na mtaalamu wa kilimo kutoka Jimbo la Zambezia, Msumbiji, Jaime Gado, alipotembelea nchini akiwa na timu ya wataalamu saba wa mpunga na mmoja kutoka Japan, kwa lengo la kubadilishana ujuzi na kujifunza kutoka kwa wakulima wa Tanzania kuhusu namna ya kuzalisha mpunga bora.

Gado alisema mbali na changamoto ya kuwa na mashine zilizochakaa na ubovu wa miundombinu ikiwemo barabara, bado mkulima wa Tanzania amekuwa na hai ya kuzalisha mpunga bora.

"Tumeona changamoto kadha, lakini bado mkulima huyu amekuwa akizalisha kilicho bora...,tatizo ni uhakika wa soko, naishauri Mamlaka husika kuangalia namna ya kumsaidia mkulima huyu ili pia aweze kuuza kwa wingi katika nchi zinazozunguka bara la Afrika," alisema.

"Nipende pia kuwapongeza Jica (Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan) kwa kuweka utaratibu wa kuongeza thamani ya zao hili kwa kusaidia kusimamia makubaliano kati ya wanunuzi na wakulima kwa wakulima wa Tanzania kupitia kwenye mradi wa Tanrice 2 kwani umekuwa mkombozi kwa wakulima wengi hususan waliopo kwenye skimu ya Lower Moshi," alisema.

Naye mtaalamu kutoka Tanzania, Shedrack Msemo, alitaja miongoni mwa changamoto wanazokumbana nazo wakulima ni miundombinu mibovu ya kuingia kwenye mashamba ya wakulima, kutokuwa na mashine bora ya ukoboaji wa mpunga pamoja na mashine za kuvunia mpunga.

JICA inatekeleza mradi wa Tanrice 2 nchini Tanzania na Proapa nchini Msumbiji na wataalamu wamekuwa wakibadilishana ujuzi kwa lengo la kusaidia kuongeza uzalishaji

# TPAWU walia michango NSSF

**Na Mary Mosha,** SIHA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Mashambani na Kilimo Tanzania (TPAWU), kimeiomba serikali kuingili kati tatizo kukatwa fedha na waajiri wao za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), ambapo fedha hizo haziwasilishwi kwa wakati kwenye mfuko.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi wenzake kwenye mkutano mkuu wa kamati ya utendaji Kanda ya Kilimanjaro, Mwenyekiti wa (TPAWU) Tawi la Relongo Estate Wilaya ya Siha, Rashid Mswaki, alifafanua waajiri hao wamekuwa wakiwakata fedha hizo kwa ajili ya mifuko mbalimbali ya kijamii ikiwamo NSSF, ili hali waajiri wao hawaziwasilishi fedha hizo kwa wakati.

"Sisi wafanyakazi wa mashambani na kilimo, tumekuwa tukikatwa fedha za mifuko mbalimbali ya kijamii kama NSSF na waajiri wetu, lakini hawaiwasilishi michango hiyo kwa wakati, jambo ambalo limetuletea usumbufu mkubwa," alisema Mswaki.

Mswaki aliiomba serikali na uongozi wa TPAWU iwasaidie kutatua tatizo hilo ambalo limegeuka kuwa mwiba kwa ustawi wa kiuchumi kwa kazi zao na familia zao.

Elius Mashmba, mwenyekiti wa TPAWU, tawi la TPC, alisema changamoto kubwa iliyoko kwa wafanyakazi wanapoumwa wakienda kutibiwa hospitalini hawapati huduma hiyo kutokana na fedha wanazokatwa kutokuwasilishwa na waajili wao.

"NSSF ni wadau wakubwa kwa wafanyakazi wa mashambani, wanapata mapato mengi kupitia kwa wafanyakazi hawa, mfanyakazi anapokuwa anaumwa anastahili na yeye apate fao la matibabu... miongoni mwa mafao wanayotoa NSSF ni pamoja na fao la matibabu, lakini mfanyakazi anapoenda kupata huduma hiyo ambayo ni stahili yake anaambiwa mchango haujatosha, kwa kweli inakatisha tamaa," alisema Mashamba.

Suzan Nkini, mwenyekiti wa vijana TPAWU Kanda ya Kilimanjaro, ameiomba serikali isaidie kuzibana taasisi ambazo zinashindwa kupeleka michango ya wafanyakazi wao kwa wakati

Akisoma taarifa ya mwaka, katibu wa TPAWU Kanda ya Kilimanjaro, Hatibu Losiando, alifafanua kuwa chama hicho kimeongeza idadi ya makusanyo kwa mwaka kutoka Sh. milioni 35 mwaka 2014 hadi kufikia Sh.milioni 120 kwa mwaka 2019.

Losiando alisema pamoja na mafanikio hayo TPAWU Kanda ya Kilimanjaro inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa gari la kuwafikia wakulima mashambani hasa kwenye maeneo ya vijijini, pamoja na vifaa vya thamani za ofisi hali ambayo imekuwa ikikwamisha utendaji kazi wa shughuli hizo.

Mwenyekiti wa TPAWU Kanda ya Kilimanjaro, Juma Mdolo, aliwataka waajiri kuendelea kuwapa fursa wafanyakazi wao kwenda kupata ujuzi ili kujenga mahusiano mazuri baina ya wafanyakazi na waajiri.

# Ni huzuni

NIPASHE JUMANNE MEI 7, 2019









## DK. MENGI

# Sauti ya kumkosa kila kona

Ukurasa 18



# Nilikuwa nasubiri nimkambidhi shati lake nililomshonea

ABDALLAH NYANGALIO



Dk. Abdallah Nyangalio

**Na Mwandishi Wetu**

MTAALAM wa kushona nguo nchini mwenye ulemavu wa kutoona, Dk. Abdallah Nyangalio, anamlilia Dk. Reginald Mengi, kwa sababu alikuwa amemshonea shati lake wiki iliyopita na alikuwa anasubiri arudi nchini ili akamkabidhi.

Nyangalio amebaki na shati hilo muhimu alilotaka kumkabidhi marehemu Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Mengi kama zawadi yake.

"Nilichukua vipimo vyake ili nimshonee shati kama zawadi ya kuanzisha tuzo za 'I Can' kwa watu wenye ulemavu, ambazo zimelenga kuvumbua vipaji tulivyo navyo," anasema.

Nyangalio ni mkufunzi wa kiwanda darasa kwa wasioona na watu wenye ulemavu wa ngozi (albino), kilichopo viwanja vya Sabasaba, jijini Dar es Salaam.

Pamoja na ulemavu wake wa kutoona, lakini anaweza kuitwa shujaa, kutokana na kazi anayoifanya licha ya ulemavu alionayo.

Wiki iliyopita, alishona shati hilo na alikuwa akimsubiri Dk. Mengi ili amkabidhi.

Tuzo za 'I Can' zilitolewa Machi 17, na mgeni rasmi alikuwa ni Makamu wa Rais, Samia Suluhu.

Nyangalio alishona shati hilo kwa muda wa siku mbili. Siku ya kwanza alilikata kwa kutumia vipimo alivyokuwa navyo na siku iliyofuata, alilishona kuanzia saa tisa alasiri hadi saa tatu usiku, akalimaliza.

"Nilipokamilisha kulishona wakati ninafanya mawasiliano na viongozi wa Dk. Mengi Foundation, ili kusudi tupange siku ya kumkabidhi, ndipo wakaniambia yupo safarini na atakaporejea, wataangalia lini wakutane naye," anasema Nyangalio.

Alhamisi iliyopita akiwa ofisini kwake, ndipo akapata habari kuwa Dk. Mengi amefariki dunia huko Dubai.

"Nilitamani kuja siku ya jana (Ijumaa) hapa nyumbani, lakini sikuweza, kwa sababu presha ya macho ilikuwa juu nilipata uchungu sana.

"Leo (Jumamosi) nimeamka angalau afadhali, nikasema acha nije kumuenzi mzee wetu, ambaye alitupenda sana walemavu, hakutubagua na alipenda tujione kama watu wengine kwenye jamii," anasema.

"Sijafanikiwa kumkabidhi Dk. Mengi zawadi yake ambayo nilimuandalia kama sehemu ya shukrani, lakini naomba ipokelewe hata kama wataamua kuiweka mahali iwe kumbukumbu."

Shati hilo amelishona kwa kutumia kitenge na lenye mikono mirefu na rangi ambazo hazichoshi macho.

"Kama ungekuwa umekuja ofisini kwangu, ningekuonyesha namna nilivyolishona. Nilitumia ujuzi wangu wote, ili akilipokea afurahi kuona kazi ya mikono yangu licha ya kwamba nina ulemavu wa kutoona," anasema.

Anafafanua kuwa, siyo mara yake ya kwanza kumshonea Dk. Mengi shati na kueleza kuwa la kwanza lilitokana baada ya kuhudhuria chakula cha mchana, ambacho kila mwaka alikuwa akikiandaa kwa ajili ya kundi la watu wenye ulemavu.

Walianza kufahamiana na Dk. Mengi tangu aanzishe hafla ya chakula kwa watu wenye ulemavu na yeye amekuwa mshiriki wa kila mara.

"Nilihudhuria katika hafla hizi za chakula cha mchana na watu wenye ulemavu kwa mara tatu mfululizo na kipindi chote nilikuwa nasikiliza hotuba zake, maneno yake yalinipa hamasa, kwa sababu alikuwa akisema mara kwa mara msililie viungo vilivyopotea au kuondoka, pambaneni na viungo vilivyobakia," anasema.

Maneno hayo yalimvutia na ndiyo yaliyomfanya aliporudi nyumbani siku hiyo (haikumbuki) akajiuliza amfanyie nini Dk. Mengi?

"Wazo likanijia nishone shati, baada ya kufanya utafiti na kupata kipimo chake nilinunua vifaa nikalishona na mwaka uliofuata nikaenda nalo Diamond Jubilee kwenye sherehe aliyokuwa ameandaa ya chakula cha mchana kwa watu wenye ulemavu nikamkabidhi," anasimulia.

> "Nilichukua vipimo vyake ili nimshonee shati kama zawadi ya kuanzisha tuzo za 'I Can' kwa watu wenye ulemavu, ambazo zimelenga kuvumbua vipaji tulivyo navyo

"Nilipomkabidhi lile shati la kwanza alifurahi sana kwa sababu niliyeshona sioni," anasema.

Sherehe za mwaka uliofuata hakubahatika kuhudhuria, lakini alipokwenda mwaka mwingine uliofuata, Dk. Mengi alimkumbuka na kumfuata alikokuwa amekaa na kumsalimia.

"Aliniambia kuwa amefurahi kuniona tena. Nilimshukuru kwa kuja kunisalimia, nilimwambia amenithamini sana na sikutegemea, alinikumbatia nilipata faraja sana," anasema.

Kuhusu sherehe za mwaka huu, Nyangalio anasema mwaka jana alikwenda mkoani Simiyu kwenye maadhimisho ya siku ya watu wenye ulemavu na huko alikutana na Mkurugenzi wa Dk. Mengi Foundation, ambaye alitangaza kuhusu tuzo za 'I Can' kwa watu wenye ulemavu.

"Nakumbuka kulikuwa na tuzo za aina tofauti ambazo tulihamasishwa tuziwanie, binafsi nilishiriki nikaandika katika kundi la kipaji cha pekee, ninashukuru Mungu nilishinda na kupewa tuzo pamoja na hundi," anaeleza.

Nyagalio anakiri Dk. Mengi aliwapenda watu wenye ulemavu, vijana na aliwataka wasikate tamaa na wauchukie umaskini.

"Alikuwa mtu wa aina ya pekee, hakuangalia mali alizokuwa nazo, alijishusha kwa kila aliyekutana naye, haijalishi wewe ni mzima ama mlemavu. Alitupenda wote bila ya ubaguzi," anasema.

Nyangalio anasema kifo chake kwake, ni pigo kubwa kwa sababu kila alipokuwa akimsikiliza alikuwa akijifunza jambo jipya.

"Nyie ni mashahidi jinsi alivyokuwa anatupenda. Ulikuwa ukikutana naye, haangalii utajiri aliokuwa nao, alijishusha na alikuwa akiongea na kila mmoja. Alisaidia watu mbalimbali, makundi mengi kwenye jamii ni wanufaike wa kile ambacho Dk. Mengi alikitoa ama kwa kutoa fedha au mchango wa mawazo."



Dk. Reginald Mengi, alipogawa chakula katika moja ya tafrija za chakula cha mchana alizokua akiziandaa maalumu kwa watu wenye ulemavu, kwenye ukumbi wa Diamond Jubilee, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Dk. Reginald Mengi (wa pili kulia), akikata keki pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi isiyo ya kiserikali inayojihusisha na watu wenye ualbino ya Under The Same Sun (UTSS), Peter Ash (wa pili kushoto), Mkurugenzi wa UTSS, Berthasia Ladislaus (kulia) na mwanafunzi Sevelyne Nocholous, katika sherehe ya miaka 10 ya kuanzishwa taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam, mwaka jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## UNDER THE SAME SUN:

# Mengi aliwekea furaha nyuso za wenye ualbino

**Na Salome Kitomari**

SHIRIKA la watu wenye ualbino (Under the Same Sun), linamkumbuka Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, kwa kuweka furaha kwenye nyuso za watu wenye ualbino na wenye uhitaji nchini Tanzania na kukubali kujitoa kwa ajili yao kwa fedha na muda ili kukamilisha furaha yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Under The Same Sun, Berthasia Ladislaus, anazungumzia mambo makubwa na mengi aliyofanya Dk. Mengi kwa watu wenye mahitaji maalum baada ya kutumia muda wake mwingi kukaa nao.

"Hakujali fedha alizonazo, wala nafasi yake na heshima yake, alitenga muda wake kukaa nao na kuwasikiliza na ndipo alijua matatizo yao na kila wakati alishiriki kuyatatua ikiwamo kuhakikisha wanapata elimu, ajira na mahitaji mengine ya maisha, ni watu wachache sana wa nafasi yake wanafanya hivi," anasema.

Kwa miaka 10 anasema wamefanya kazi na Dk. Mengi kwa karibu sana na kila wakati aliwatatulia shida zao na kukubali kuwasaidia watu wenye ualbino.

"Mara ya kwanza tulimwalika kwenye hafla yetu mwaka 2013 na mwaka huu Februari, wakati tunaadhimisha miaka 10 ya shirika, alikubali kuja kuwa mgeni rasmi na alishiriki mwanzo hadi mwisho.

"Tunakumbuka siku hiyo watu, vijana wenye ualbino, walimweleza changamoto za kupata nafasi ya mafunzo kazini kwa vitendo, ajira, elimu. Naye aliwakumbatia, aliongea nao na kuahidi kuwapa nafasi kwenye kampuni zake," anaeleza.

> **Dk. Mengi alikuwa na moyo wa upendo kwa kila mtu na hakuwahi kumbagua yeyote bali aliangalia utu wa mtu. Alitenga muda wa kuongea naye na kujua changamoto zake**

Ladislaus anasema, asasi yao itamkumbuka kwa jinsi alivyowapa nafasi ya matangazo bure kwenye vyombo vyake vya habari, mfano kila kabla ya taarifa ya habari alitoa tangazo lao la kuelimisha jamii kuhusiana na ualbino na ilisaidia sana kuwafikia Watanzania wengi kwa wakati mmoja.

**Kampuni zawahudumia**

Tulitangaza mara tatu hadi tano bila kutoa fedha yoyote na ilitusaidia sana kuzuia ukatili dhidi ya watu wenye ualbino, lakini kwenye magazeti ya The Guardian na Nipashe, walipata nafasi bure ya matangazo na habari zao kuandikwa.

Anakumbuka mwaka 2009, walitangaza bure kwenye magazeti ya The Guardian na Nipashe. Hiyo ilihusu nafasi za ajira na elimu kwa wenye ualbino. Waliwapata watu wengi sana na yote hayo ni matunda ya msaada wa Dk. Mengi.

Anasema Dk. Mengi ameacha urithi mwema kwa jamii. Amegusa maisha ya watu wenye ualbino na watu wa hali ya chini kwa kiasi kikubwa.

Mkurugenzi huyo anasema, wapo walioajiriwa kwenye kampuni zake na wengine aliwasomesha, yote yakitokana na moyo wake wa upendo.

**Aliwafanya rafiki**

"Dk. Mengi alikuwa na moyo wa upendo kwa kila mtu na hakuwahi kumbagua yeyote bali aliangalia utu wa mtu. Alitenga muda wa kuongea naye na kujua changamto zake yote. Hiyo ni kutaka kuweka furaha kwenye uso wa mtu, anaeleza Mkurugenzi Ladislaus.

Anaeleza kwamba, siyo kila mwenye uwezo wa fedha, wenye nafasi kubwa anasaidia, lakini kwa Dk. Mengi ni jambo lililokuwapo kwenye moyo wake.

Aliandaa chakula cha pamoja na watu wenye mahitaji maalum, alitenga muda wa kukaa nao na kuzungumza nao na ndiko kulimwezesha kujua changamoto zao.

Ladislaus anasema, Dk. Mengi alitumia nafasi ya ushawishi alionayo kutetea watu ambao sauti zao hazikusikika.

Ilikuwa ni ajenda iliyo ndani ya moyo wake. Aliwaajiri kwenye kampuni zake na mengine mengi aliyafanya kwa moyo wake wote.

"Huu ni msiba wa taifa na hasa watu wenye mahitaji maalum. Under The Same Sun alitulisikiliza bila kuchoka na kutusaidia na wakati mwingine alitutafuta kutuuliza tunahitaji msaada gani."

Kwa kweli, pengo lake halizibiki, wapo wenye uwezo, lakini hawakufanya kama alivyofanya Mwenyekiti, hawana unyenyekevu kama wake na hawasaidii jamii.

Dk. Mengi alipanda mbegu katika mioyo ya wanajamii wenye mahitaji, tutamkumbuka kwa kasi kubwa ya kuweka furaha kwenye nyuso za watu wengi, kujitoa kusaidia watu wengi sana.

"Tunaamini kampuni zake zitaendelea kumuenzi na kupanda mbegu endelevu."

Anasema serikali ina nafasi kubwa kuifanya jamii itambue na kuwasaidia watu wenye ulemavu, kuna sheria ya watu wenye mahitaji maalum, lakini bado inahitajika kuelimisha jamii kuwa mstari wa mbele kusaidia kundi hilo na hasa kwa wenye uwezo wa kifedha.

"Mengi hakuwaona kuwa ni kero kwao, alikaa nao na kujua changamoto zao, unajua mtu mwenye ualbino au ulemavu anapitia changamoto nyingi ambazo wakati mwingine humfanya kuwa mwenye hasira.

"Usipomjua unaweza kumchukia, ukikaa nao karibu wanafurahi sana na inawasaidia kisaikolojia kuwa kuna mtu amewajali," anasema Ladislaus.

Anasema, serikali inaweza kuwa sehemu ya kusaidia wenye ulemavu kwa kutoa msamaha wa kodi kwa kundi hilo na ingesaidia sana kupunguza changamoto na hasa ukali wa maisha.

Pia, anaziasa taasisi za kidini ziwakumbushe waumini wao umuhimu wa kusaidia wahitaji kama wenye ualbino na wenye ulemavu.

"Nimefanya kazi na watu wenye ualbino, nikagundua wengi wana historia tofauti za maisha ikiwamo unyanyapaa. Ni wenye simanzi ambazo zilianza toka utotoni.

"Lakini, kwa kuzungumza na kukaa nao karibu, wanajiona nao wana haki kama watu wengine na hilo ndilo ambalo Dk. Mengi alilifanya kila wakati."

Anasema wenye ualbino, changamoto kubwa hasa kwenye uelewa wa jamii kuwaona wao ni watu tofauti na wengine.

"Tunawaeleza kuwa mwenye ualbino ni binadamu kama mwingine. Kilichosababisha yeye kuwa hivyo, ni vinasaba vya mzazi mmoja ndiyo maana ngozi, macho viko tofauti na wana uoni hafifu, hivyo hawawezi kukaa juani.

'Hatari iliyopo kwa sasa ni ufukuaji wa makaburi ya wenye ualbino na kwa sasa hili ni tukio la nne kutokea mkoani Mbeya. Sasa tunatoa elimu kwa wananchi mkoani humo ili wajue albino ni binadamu kama wengine.

"Wameanza kufukua makaburi ya wenye ualbino, wanachukua viungo kwa lengo la kutafuta utajiri. Tunawaelimisha sana, tunachoona kwa sasa ni kuwa wamekosa walio hai sasa wanavamia makaburi yao," alisema.

# Mbatia aeleza siri ya Dk. Mengi 'How not to die'



James Mbatia,

> **Nakumbuka aliniambia kuwa bado ana nguvu na alinishirikisha kwa kuniambia kuwa afya yake ni njema kabisa**



Dk. Reginald Mengi (kulia), aliposaini kitabu chake kiitwacho 'I Can, I Must, I Will', kilichonunuliwa baada ya uzinduzi wake, uliofanyika, jijini Dar es Salaam Julai 2, mwaka jana. **PICHA: JOHN BADI**

**Na Romana Mallya**

MACHI 14, mwaka huu, nilikwenda nyumbani kwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, kwa ajili ya chakula cha jioni. Katika mazungumzo yetu alinileteа kitabu kilichoandikwa 'How not to die' na kunieleza kuwa alikuwa akikisoma na kuniahidi atakapokimaliza atanipa ili nikisome."

Ni kumbukumbu ya Mbunge wa Vunjo (NCCR Mageuzi), James Mbatia, alipokutana na Dk. Mengi nyumbani kwake kwa mara ya mwisho.

Anasema alimfahamu Dk. Mengi kwa utajiri wa hekima, busara na unyenyekevu aliouchota kutoka kwake.

Dk. Mengi kwake alikuwa mwalimu, baba na rafiki.

Sababu ya kumbukumbu ya maongezi yake ya mwisho na Dk. Mengi kuhusu kitabu hicho alichoahidiwa, lakini hakubahatika kukabidhiwa ni kuwa siku hiyo wakiwa wameketi sebuleni nyumbani kwa Dk. Mengi, Kinondoni, jijini Dar es Salaam, walizungumza mambo mengi mbalimbali kuhusu maisha yake.

"Nikiwa nimekaa pembeni yake yeye akiwa amekaa kwenye kiti chake anachokipenda kile pale (anakionyesha), wakati tunazungumza alinyanyuka na aliporudi alikuwa ameshika kitabu,"anaeleza.

Mbatia anasema alikinyanyua kitabu hicho na kumuonyesha ujumbe ulioandikwa.

"Aliniambia unakiona hiki kitabu 'How Not to Die' namna gani ya kutokufa, wakati huo akinionyesha tulikuwa na wanafamilia wengine, nakumbuka akaniambia akishamaliza kukisoma atanipa nami nikisome."

Anasema sababu ya kumletea kitabu hicho ni kutokana na yeye kumuuliza Dk. Mengi anawezaje kuanzisha kampuni mpya na umri alionao pamoja na maradhi yaliyokuwa yanamkabili na anapata wapi nguvu ya kuanzisha kampuni hizo na alimjibu kuwa siri ipo kwenye kitabu hicho.

"Nakumbuka aliniambia kuwa bado ana nguvu na alinishirikisha kwa kuniambia kuwa afya yake ni njema kabisa," anasimulia.

Anasema Dk. Mengi alimwambia mguu uliokuwa unamsumbua anauona siyo tatizo kwa sababu afya yake kwa mujibu wa ripoti ya daktari ilikuwa inaimarika.

"Tena tulikwenda mbali zaidi mpaka ikafikia hatua tukaahidiana tuanze 'diet' ijulikanayo kama 'Keto diet' tulikubaliana kuwa atakayepungua kwa kiwango walichokubaliana atapata zawadi."

Alimwambia anatarajia kwenda Rwanda kukutana na Rais Paul Kagame kwa ajili ya kufanya naye mazungumzo ya biashara zake zilizopo nchini humo.

"Sijajua kama alikwenda Rwanda ama la, kwa sababu wakati tunazungumza aliniambia anataka kwenda kumuona Rais Kagame kwa mazungumzo zaidi," anaeleza.

Mbatia anataja jambo lingine ambalo siku hiyo Dk. Mengi alimshirikisha ni kuhusu suala la watu wenye ulemavu.

Anamnukuu: "James Mwenyezi Mungu akikupa nguvu zitumie, mimi ni bomba la kupitishia tu sibaki navyo, ninachopata nawapa na wengine, kwa nini ninasaidia watu wenye ulemavu ni ili kukuza utu wao, kuwapa heshima kama binadamu wengine wajisikie kwamba na wao ni binadamu."

Anaeleza kuwa alimwambia mwaka huu ameanzisha mashindano ya tuzo mbalimbali kwa watu wenye ulemavu na alimtaka awe mmoja wa watoa tuzo kwa washindi.

Tuzo hizo za `I Can' zilitolewa Machi 17, kwa makundi mbalimbali, mgeni rasmi akiwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu.

"Nilipewa nafasi ya kutoa tuzo ya mwanasiasa bora ambayo ilikwenda kwa Amina Mollel," anasema.

Anasema wakati wakizungumzia masuala ya watu wenye ulemavu alimuuliza kwa nini wanaitwa walemavu wa viungo.

"Aliniambia kuwa umaskini wa fikra ni mkubwa Tanzania na anauchukia sana, nakumbuka nilimwambia kuwa ninaamini tuna umaskini mkubwa wa ulemavu. Wakati natoa tuzo hii nilimshukuru Dk. Mengi kwa kulinda, kutetea na kudumisha utu, heshima na haki za msingi za watu wenye ulemavu," anasema.

Mbatia anarejea kunukuu maneno aliyosema siku hiyo ya tuzo kuwa: 'Wale wanaoona wanaviungo vilivyokamilika na kuwaita wale ni walemavu, sisi tulio wengi tuna ulemavu mkubwa wa fikra kuliko wale.' Maneno haya yalinijia kutokana na mjadala mrefu tuliofanya siku ile hapa nyumbani kuhusu walemavu," anasema.



Dk. Reginald Mengi (L), aliposalimiana na Rais Mstaafu wa Nigeria, Jenerali Olusegun Obasanjo, walipokutana katika Mkutano wa Eneo la Biashara Huru Barani Afrika, ulioandaliwa na Umoja wa Afrika (AU), mjini Kigali Rwanda, Machi 21 mwaka jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Mbatia anasema kwenye mijadala walioifanya tangu mwaka huu uanze, Dk. Mengi alionyesha kuwa ana nguvu kubwa ya kuendelea kulitumikia taifa la Tanzania.

"Dk. Mengi alikuwa na nguvu kubwa ya maono, maono yake yalikuwa ni ya zaidi ya miaka 25 hadi 30 ijayo, hii ndiyo siri ya 'How not to die'," anasema.

Anasema matendo mema aliyofanya Dk. Mengi duniani ni sauti huru na hai na anaamini licha ya kwamba kimwili hata kuwapo, lakini sauti huru na hai itaendelea kuwapo.

"Ukisoma kitabu chake cha I Can, I Must, I Will ambacho kilikuwa kimeshatafsiriwa kwa Kiswahili, nakumbuka kuna siku tulikutana akaniambia, kijana wangu James nakuomba ukisome hiki kitabu ukihariri vizuri kabla hakijachapishwa."

Kitabu cha I Can, I Must, I Will kilizinduliwa Julai 2, mwaka jana na Rais Dk. John Magufuli.

Kitabu hicho kilikuwa kimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza na katika hotuba yake siku hiyo Dk. Mengi alimuahidi Rais Magufuli kuwa, watafanya mchakato wa kukitafsiri ili ujumbe aliouandika uwafikie Watanzania wote.

"Aliniomba nisome kitabu chote baada ya kutafsiriwa kabla ya kuingizwa sokoni ili kuangalia kama kuna sehemu ya kurekebisha. Hivi tunavyoongea kitabu kipo kwenye mchakato wa kutolewa."

Mbatia anasema kila akitumia ulimi wake anamkumbuka Dk. Mengi kwa sababu moja ya wosia wake kwake ambao alikuwa akiutoa mara kwa mara ni kwamba maisha yapo kwenye ulimi.

Jambo la pili atakalo mkumbuka anasema ni kuondokana na dhana kwamba Watanzania ni maskini, suala ambalo hakupenda vijana waliamini.

"Aliniambia ukihubiria sana vijana kuwa ni maskini, midomo huumba, sisi siyo maskini, aliniambia kuwa hata biblia imeandika 'Watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa'.

"Binafsi hili nitajitahidi sana kuliishi kutowaita Watanzania ni maskini, lazima tuwe na mawazo mapana ili kuisaidia nchi kupata maendeleo."

Katika jambo la tatu atakalomkumbuka ni kufanya kazi kwa bidii bila kukata tamaa na unaifanya kwa ajili ya maslahi mapana siyo kwa ajili yako mwenyewe.

"Unafanya kazi kwa bidii bila kujiona bora kuliko wengine, jambo la nne ni kuondoa ubinafsi na kujiona jeuri kwa sababu ya mamlaka uliyopewa, unatakiwa kuweka utu mbele zaidi kuliko kitu kingine chochote, kuheshimu utu wa binadamu zaidi kuliko kitu kingine chochote."

Jambo la mwisho ni unyenyekevu, "alinisisitiza sana kwa kuniambia kijana wangu ukipenda kuheshimiwa lazima uwe mnyenyekevu."

## NIFE KAMA MENGI

WAPO walokwishaanza, kusema maneno mwingi,
Wakisema nimeanza, kuvuta-vuta 'vishungi',
Mauti kuyapa-inza, kuyaveshea ushungi,
Ila kwangu sijivungi, acha nife kama Mengi.

Kaa kitako naanza, kweleza mema ya Mengi,
Najua utajifunza, kwa kutoniona pungi,
Penginepo uki-kinza, takuwa ja purutangi,
Nafuliliza kuwaza, acha nife kama Mengi.

Jinsi alivyozi-sunza, mali kwa kina Msangi,
Ziwe pesa na machenza, aligawa bila mbungi,
Hakupendelea chonza, kuuharibu u Mangi,
Ndiyo maana nasema, acha nife kama Mengi,

Walo wengi wamefyonza, mali na zake shilingi,
Wamesomeshwa la kwanza, tangu shule za msingi,
Hadi chuo kiwatunza, mahari kawapa nyingi,
Kwa nini siwaze hivi? Acha nife kama Mengi.

Wale waishio Mwanza, kule kwa akina Kangi,
Wengine kutoka Nyanza, walifaidi finingi,
Bila Mengi kuwatunza, wangeliitwa 'mabangi',
Mengi Mungu amtunze, acha nife kama Mengi.

Serengeti liwa-kanza, waje wawe ja vigingi,
Kaasa waepe manza, wasitamani milungi,
Wacheze mpira kwanza, wahofu sana farangi,
Leo hayupo 'kasepa,' acha nife kama Mengi.

Nani tutam-enenza, kwa matendo hata rangi?
Wapi alipojibanza? Apachukue pa Mengi,
Simwoni nimesha-enza, wa kumvalisha yungi,
Nitakukumbuka sana, acha nife kama Mengi.

Wewe lipi tuku-enza? Kubwa na lenye msingi,
Kwa watu ulolifanza, mojawapo kama Mengi,
Au umekuwa funza, si mtu wa watu wengi?
Nikumbukwe japo moja, acha nife kama Men
Yalosalia na panza, atamaliza Msengi,
Nawahi weka kiunza, msibani watu wengi,
Yatosha niliyo-ganza, kwa heri kipenzi Mengi,

**Adam Mwambapa**

**TUTAONANA KWA MOLA, ACHA NIFE KAMA MENGI!**







HUZUNI 1942 - 2019

# Dk. Kimei asimulia alivyomuomba kazi

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI mstaafu wa Benki ya CRDB, Charles Kimei, anasema alikutana kwa mara ya kwanza na Dk. Reginald Mengi, alipokwenda kumuomba kazi ya kuwa mshauri kwenye kampuni yake.

"Yeye ndiye aliyefanikisha ndoto yangu hadi kufikia kushika nyadhifa ya juu niliyostaafu nayo mwanzoni mwa mwaka huu."

"Nimefika hapa nilipo kwa sababu ya ushauri mzuri niliopata kutoka kwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, ambaye nilipomwendea kwa mara ya kwanza kwa ajili ya kumuomba kazi ya kuwa mshauri (consultant), alinishauri ili niweze kuifanya kazi hiyo vizuri lazima nipate uzoefu wa kufanya kazi serikalini."

Januari 26, mwaka huu, Dk. Kimei aliiaga rasmi Benki ya CRDB baada ya utumishi wake wa zaidi ya miaka 20.

Akiwa miongoni mwa waombolezaji mbalimbali waliofika nyumbani kwa marehemu Dk. Mengi kuhani msiba wake uliotokea nchini Dubai, Falme za Kiharabu, anasema alikutana naye mara ya kwanza miaka ya 70 wakati alipokuwa akitafuta kazi baada ya kuhitimu masomo yake.

Katika pilikapilika za kutafuta kazi, alikutana na Dk. Mengi na kikubwa alichomuomba ni kupata nafasi ya kuwa mshauri kwenye moja ya kampuni zake.

Anasema alipomaliza masomo alitamani kufanya kazi hiyo, lakini alipokutana na Dk. Mengi, alimshauri asifanye kazi hiyo kabla ya kupata uzoefu serikalini.

"Nakumbuka alinishauri kuwa kabla ya kufanya kazi hiyo lazima nihakikishe kuwa nina uzoefu na alinishauri nitafute kazi serikalini au kwenye taasisi za umma."

"Tuliongea kwa kirefu sana na aliniambia sababu ya ushauri wake ni kunitaka kufahamu watu, nielewe mlolongo wa kufanya maamuzi, nakumbuka alinihoji kwa nini nisiende Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

"Nilichomjibu ni kwamba sijajaribu kuomba kazi BoT, lakini nilifanyia kazi ushauri wake na nikaomba kazi BoT na kupata na mwishoe nikafika nilikofika." anasimulia

Katika maisha yake anasema hajawahi kuacha kukumbuka mchango wa ushauri wa Dk. Mengi kwake kwa sababu kwa sehemu kubwa umemsaidia kimaisha.

"Nikiri kuwa taaluma yangu kwa kiwango kikubwa Dk. Mengi ndiye aliyeitengeneza kwa sababu baada ya kwenda kumuomba nifanye kazi ya mshauri, aliona njia ninayokwenda nayo siyo sahihi kwa wakati huo na kuniongoza njia ya kupita ambayo leo najivunia kwa mafanikio niliyoyapata," anasema.

Baada ya kwenda CRDB anasema alikutana tena na Dk. Mengi ambaye alikuwa ni mwana




Dk Charles Kimei, . **PICHA ZOTE: MAKTABA**

> **Nikiri kuwa taaluma yangu kwa kiwango kikubwa Dk. Mengi ndiye aliyeitengeneza kwa sababu baada ya kwenda kumuomba nifanye kazi ya mshauri, aliona njia ninayokwenda nayo siyo sahihi kwa wakati huo na kuniongoza njia ya kupita ambayo leo najivunia kwa mafanikio niliyoyapata,**



Mwenyekiti Mtendaji wa IPP Media, marehemu Dk. Reginald Mengi, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Tanzania Saccos For Women Entrepreneurs (TASWE – Saccos), uliofanyika katika ukumbi wa St. Peter's jijini Dar es Salaam Septemba 10 2016. Kulia ni Mwenyekiti wa TASWE Saccoss, Mama Anna Matinde na Balozi Mdogo wa India, Baluinder Humpal. **PICHA: MAKTABA**

# Dk. Kimei asimulia alivyomuomba kazi

**INATOKA UK.18**

hisa mkubwa kwenye benki hiyo.

"Katika kipindi changu chote nilichokuwa Benki ya CRDB, tulifanya kazi naye vizuri. Kama unavyojua mwana hisa huwa hakai kwenye bodi, hivyo Dk. Mengi aliweka mjumbe wake, tuliwasiliana mara nyingi na kama kulikuwa na jambo alikuwa ananipigia simu tunashauriana, huyu ndiye Dk. Mengi."

Anasema kila alipozungumza na Dk. Mengi alikuwa akijifunza vitu vipya ambavyo vilimwezesha kufanya kazi yake kwa ufanisi mkubwa. "Katika vitu ambavyo sitavisahau ni namna alivyonijenga kujiamini na kufanya kazi kwa bidii na kwa kujua kuwa kuna watu ambao wanaelewa kazi za benki hivyo zisiingiliwe."

Ushauri alioupata toka kwa Dk. Mengi unamkumbusha na yeye kuwaasa vijana kujifunza wanapotaka kwenda safari ndefu yenye mafanikio hawawezi kwenda wenyewe.

"Binafsi nilijifunza hiki kitu kutoka kwa Dk. Mengi, huwezi kwenda safari ndefu peke yako, lazima ushirikiane na watu wengine," anasema na kuongeza:

"Nendeni wengi au angalau wawili. Dk. Mengi ameweza kufanya mambo mengi kwa sababu aliwathamini watu, aliwaamini na alitembea na watu wengi bila kujali watu hao wametokea wapi, wana mwelekeo gani, yeye alikwenda nao na ameenda mbali sana," anasema.

Alitoa mfano kampuni za Dk. Mengi na kueleza kuwa kwa sababu aliamini kuwa safari ya mafanikio ni kwa kuruhusu kutembea na watu wengi, walioachwa wataziendeleza na kufikia mafanikio zaidi.

"Ninafahamu Dk. Mengi, ameacha warithi wazuri na imara kwenye kampuni zake, ili kuwa imara ni lazima iwe na watu ambao wanajielewa, wanajua madhumuni ya taasisi, wajue ni kitu gani wanafanya na wakashirikisha wafanyakazi wote ili nao wayajue na kuyatekeleza."



Rais Dk. John Magufuli akimkaribisha Dk Reginald Mengi Ikulu .

**"Binafsi nilijifunza hiki kitu kutoka kwa Dk. Mengi, huwezi kwenda safari ndefu peke yako, lazima ushirikiane na watu wengine**



"Mara nyingi unapokuwa mwenyekiti wa kampuni ambayo ni yako mwenyewe ukawaachia wengine waendeshe ni kitu cha ajabu sana. Dk. Mengi ni jasiri na mwenye kujua uongozi wa kampuni unavyokwenda. Wengi wanataka kukaa karibu wasimamie wenyewe tu kila kitu wanaogopa kupoteza, ila Dk. Mengi hakuogopa, aliwaachia kila kitu kikaendeshwa na wataalam."

Akitoa mfano Benki ya CRDB, Dk. Kimei anaeleza kuwa kwa sababu alitengeneza timu nzuri, ndiyo maana yale aliyoyaacha yanaendelezwa na benki haijasambaratika.

"Tuliwajenga wafanyakazi wajione kuwa benki ni kama yao hata mfanyakazi wa kawaida ukimuuliza hii benki ni ya kina nani, atakujibu ni yetu, hasemi ni ya wananchi, anasema ni yetu, nikiangalia kampuni za Dk. Mengi mfano ITV natumaini wafanyakazi wanasema ITV ni yetu."

"Hata kama yupo au hata akikaa miaka mingi hajaja kuwaona bado ni yenu. Ninaamini timu aliyoiacha kwenye kampuni zake itaimarika zaidi kuliko ilivyokuwa."

Anasema anajivunia kukutana na Dk. Mengi kwa sababu amemfundisha kwenye masuala yanayohusu uongozi, namna gani ya kushirikiana na watu.

"Nyie ni mashahidi licha ya utajiri aliokuwa nao, lakini hakuwabagua watu kulingana na vipato vyao, alikuwa akikutana na mtu awe mdogo au mkubwa, awe tajiri au maskini alikuwa anakuchukulia kama yeye alivyo, hiki ndiyo kitu ambacho watu wengi hatuna hasa walio na nafasi.

Nilichojifunza kutoka kwa Dk. Mengi ni kwamba hata ukiwa kwenye ngazi ya juu namna gani lazima uwaheshimu wengine bila kujali wana hali gani kimaisha, awe maskini au tajiri, unapaswa kuheshimu utu wake.

Aliyaomba makundi mbalimbali ambaye Dk. Mengi enzi za uhai wake amekuwa akiyasaidia, kumuenzi kwa kufanya kazi kwa bidii ili kuondokana na umaskini.

Ninawataka wajue, Dk. Mengi ametutangulia na ni majonzi, lakini wajue yote ni kazi ya Mungu na ataendelea kuwapa nguvu na kuwasaidia pale wanapokuwa wanahitaji msaada, tufurahi kwamba ameondoka kwa heri na amani, ninaamini kwamba Mungu ameilaza roho yake mahali pema peponi.

Ameondoka kwa namna ambayo hata tulivyokaa hapa nyumbani kwake tunasema yupo au hayupo. Mimi ukiniuliza naona kama bado yupo, naamini yupo tutakutana naye huko mbele.

Dk. Kimei amewataka vijana wamuenzi Dk. Mengi kupitia kitabu chake cha I Can, I Must, I Will kwa kuondokana na umaskini, kwa kuwa na macho yanayoona fursa na kuamini kila kitu kinawezekana haijalishi wanamitaji ya kiasi gani.



Aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania (MOAT), Dk. Reginald Mengi (wa pili kulia), Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Bahame Nyanduga (kushoto), Rais wa MCT, Jaji Thomas Mihayo (wa tatu kulia), na Mjumbe wa Bodi ya MCT, Jaji Juxon Mlay wakifuatilia utoaji wa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2015, zilizoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na washirika wake, jijini Dar es Salaam April 29.2016. **PICHA: JOHN BADI**



## HUZUNI 1942 - 2019

### BBC WAOMBOLEZA:

# Si rahisi kumpata kama Dk. Mengi

## ●Salim Kikeke akumbukanasaha zake ITV, aliko sasa

IMEKUWA wiki ya majonzi kwa Watanzania na majirani zake, baada ya kupokea taarifa ya kifo cha Dk. Reginald Mengi, kilichotokea Dubai, katika Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Amefariki dunia, akiwa na umri wa miaka miaka 77.. Wengi wanamkumbuka kwa kuwa mfanyabiashara mahiri na mmiliki wa kampuni ya IPP Limited na IPP Institute of Technology and Innovation.

Huku Watanzania wakijiandaa kumpumzisha, baadhi wanajiuliza iwapo Tanzania itampata mtu atakayeweza kuziba pengo aliloliacha.

Lakini, cha kujuliza kwa undani, Dk. Mengi alikuwa ni mtu wa aina gani?

**Mtu wa watu**

Dk. Mengi amekuwa akijitoa katika kusaidia wasio nacho na wenye uhitaji kwenye jamii, ikiwemo walemavu wa ngozi na kugharamia matibabu ya watoto wenye matatizo ya moyo nchini India.

Kila mwaka, Dk. Reginald Mengi, alijiwekea utaratibu wa mwaka mpya unapoingia, alikuwa akiandaa chakula cha mchana kula na wenye ulemavu wa kila aina nchini Tanzania, kitu ambacho hakitasahaulika miongoni mwa Watanzania:

Ukarimu wake kwa watu wenye ulemavu ni miongoni mwa sifa zinazoendelea kuenziwa kwa Dk.Mengi.

Aliweza kuwa na maelewano mazuri na watu wa tabaka mbalimbali, wakiwamo wanasiasa wa kada mbalimbali, hivyo kuvuka mipaka ya uhasama wa kisiasa baina ya kambi mbalimbali za kisiasa nchini Tanzania.

Kiongozi wa chama cha upinzani cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, anasema anaamini kwamba Dk. Mengi alikuwa na mchango mkubwa katika kukuza demokrasia nchini Tanzania

'' Ni mtu ambaye alipoona kuna jambo halali la kushughulikiwa kwa ajili ya manufaa nchini, alikuwa anazungumza moja kwa moja na wa pande zote kuhakikisha jambo hilo linatendeka. Alikuwa na mchango mkubwa kabisa katika kuhakikisha kunakuwa na demokrasia nchini,' anasema Zitto Kabwe.

Si Tanzania pekee alikofahamika na kupendwa na watu mbalimbali waliotambua kazi zake na mchango wake katika maendeleo ya nchi yake na maisha ya Watanzania kwa ujumla.

Imedhihirika baada ya kifo chake, kwani watu kutoka mataifa na tabaka mbalimbali, wamemwagia sifa kwenye mitandao ya kijamii husuan kupitia' Twitter.'

**Hakukata tamaa**

Waliomfahamu Dk. Mengi wakati wa uhai wake, wanasema hakuwa mtu wa kukata tamaa. Wakati



Salim Kikeke, mtangazaji wa BBC, aliyetokea mikono ya ITV, akumbuka sentensi nzito za Dk. Mengi, kabla na baada ya kuondoka ITV. **PICHA: BBC**.

> **Ni mtu ambaye alipoona kuna jambo halali la kushughulikiwa kwa ajili ya manufaa nchini, alikuwa anazungumza moja kwa moja na wa pande zote kuhakikisha jambo hilo linatendeka**

mambo yalipoonekana kwa wengine ni magumu, alitumia fursa hiyo kujitafutia suluhu ya kibinafsi, pia kutoa suluhu kwa matatizo ya jamii nzima ya Watanzania.

Mfano Mwaka wakati Tanzania ilipokumbwa na uhaba wa bidhaa karibu zote, kati ya miaka ya 1983 1984, alihangaika kupata kalamu ya kuandikia.

Dk. Mengi aliamsha ari yake ya ujasiriamali na akaamua kuanza kuagiza bidhaa kutoka nchi jirani ya Kenya. Miongoni mwa bidhaa za kwanza alizoziagiza ni kalamu za wino kutoka Mombasa Kenya.

"Wakati mizigo ulipowasili sikujua niuweke wapi. Kwa hiyo, mahali pasuri pa kuiweka palikuwa ni chumbani kwangu. Ilikuwa katika chumba kile ambako nilianza kupanga kalamu zangu," aliliambia jarida la Forbes Africa, toleo la Julai 2014.

Pia, ana simulizi ya kukosa mkopo wa Dola za Marekani 4,000 (Sh. milioni 9.2) kutoka iliyokuwa benki nchini Tanzania, lakini hakukata tamaa. Aliamua kuzungumza na wafanyabiashara wenzake nchini Kenya na baadaye akapata fedha hizo.

Wakati serikali ilipokabiliana na kuwakamata wafanyabiashara ikiwashutumua kuuza bidhaa muhimu kiholela, Dk. Mengi hakuacha biashara, aliamua kupanua biashara zake katika maeneo mengine, ikiwamo kuanzisha kiwanda cha vinywaji vya Coca-Cola mjini Moshi, kilichoitwa Bonite Bottlers, Mwaka 1987.

Aliuza dawa za kusafisha viatu zilizotengenezwa kwa mkaa na mafuta na vipodozi vya kusugua mwili asilia, vitokanavyo na matope ya baharini

Dk. Mengi aliendelea kutengeneza kila bidhaa zingine akianzia na karatasi za usafi wa maliwato, sabuni, kemikali za usafi, vitanda na dawa za meno.

**Tasnia Habari**

Baadaye, Dk. Mengi aliamua kujitosa katika uwekezaji katika tasnia ya habari na kumiliki vyombo vya habari mbalimbali, vikiwemo magazeti, redio na televishen vilivyompatia umaarufu mkubwa.

Hivyo ni vya televisheni, redio na magazeti, vilivyotoa mchango mkubwa wa ajira na kukuza vipaji vya kwa waandishi wa habari nchini Tanzania.

"Kwa kweli naweza kusema hapa nilipofika sasa ni kutokana na Mengi. Nimepitia mikononi mwake nilipokuwa nafanya kazi katika kituo chake cha televisheni cha ITV.

"Hata nilipokuja huku Uingereza, aliniruhusu na baadaye aliniuliza iwapo nitarudi kufanya kazi Tanzania kufanya kazi ITV? Nikamwambia bado ninafanya kazi hapa, lakini akashauri kuwa iwapo ningependa kuendelea kufanya kazi BBC ni sawa tu niendelee.

"Kwa kawaida si waajiri wengi watakaokuambia uendelee kufanya kazi ulipo, huku wakiona una kipaji na unawaponyoka," alisema Salim Kikeke, mwandishi wa televisheni ya Kiswahili ya BBC - Swahili Dira TV.

Salim anaendelea: "Kitu kingine nilichojifunza kwake ni kwamba, japo alikuwa mtu tajiri mwenye mafanikio na umaarufu, lakini hakujikweza, Alikuwa ni mtu wa watu, hilo nimejifunza kutoka kwake."

• **Ni makala maalum ya BBC kumuenzi Dk. Rerginal Mengi, iliyotolewa katika taarifa zake.**



Mwenyekiti Mtendaji wa IPP Ltd, marehemu Dk. Reginald Mengi, akizungumza na Balozi wa China hapa nchini, Wang KE, alipomtembelea ofisini kwake, jijini Dar es Salaam Mei 18 mwaka jana. **PICHA: JOHN BADI**



# Maambukizi ya Ukimwi kwa vijana 40% kila mwaka

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA kuwa asilimia 40 wanaopata maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi nchini ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 24, hivyo kulifanya kundi hilo kuwa katika hatari zaidi ya kuangamia.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi (Tacaids), Dk. Leonard Maboko, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya uzinduzi wa programu maalumu ya usikilizaji wa vipindi vya redio kwa vijana inayotarajiwa kufanyika leo mkoani hapa.

Dk. Maboko alisema utafiti wa viashiria vya Ukimwi (THIS) uliofanyika mwaka 2016 na 2017, unaonyesha watu wazima 72,000 wenye umri kuanzia miaka 15 wanapata maambukizi mapya kila mwaka, lakini changamoto kubwa ni kwa vijana.

Alisema pamoja na kwamba changamoto ya maambukizi mapya ni kubwa zaidi kwa vijana, lakini wa kike ndio wanaochangia asilimia kubwa zaidi kwa kuchukua asilimia 80 ya maambukizi yote.

Alisema kutokana na changamoto hiyo, ndio maana wameamua kuanzisha vipindi vya redio ambavyo vitalenga kuwaelimisha vijana kuhusu namna ya kujikinga na maambukizi ya VVU na magonjwa ya ngono.

"Vipindi hivyo vitawahusu vijana ambao wapo mashuleni na wasio mashuleni, vitahusu pia masuala ya utoro mashuleni, ukatili wa kijinsia, mimba zisizotarajiwa, upungufu wa damu na usafi wakati wa hedhi kwa vijana wa kike," alisema Dk. Maboko.

Alisema wanalilenga kundi hilo ili kuliwezesha kuvuka salama katika kipindi cha mpito na kuingia kwenye utu uzima, huku akisema kuwa asilimia 27 ya wasichana wanakuwa wamepata ujauzito ama kupata mtoto kati ya miaka 15 na 19.

Alisema programu hiyo maalumu ya vipindi vya redio itafanyika katika Halmashauri nane za mikoa ya Mbeya, Njombe, Iringa na Songwe kwa kuwa ndiyo mikoa yenye maambukizi zaidi nchini.

Alizitaja Halmashauri zitakazohusika ni Rungwe na Mbarali kwa mkoa wa Mbeya, Ileje na Mbozi (Songwe), Njombe na Makete (Njombe )pamoja na Mufindi na Iringa (Iringa).

Aliwaomba wadau kushiriki katika kuhakikisha programu hiyo inafanikiwa na kuwafikia vijana wengi ili kuwaokoa na vihatarishi vyote vinavyowakabili.

Ofisa Mradi wa Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (Unicef) kitengo cha Ukimwi na Mtoto, Alice Ijumba, alisema wanakusudia kuwafikia zaidi ya vijana 300,000 katika mikoa hiyo.

# RC Chalamila aruka kiunzi soko la dhahabu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amekwepa jaribu la kutumbuliwa baada ya kutekeleza agizo la Rais John Magufuli la kuanzisha soko la dhahabu katika mkoa huo ambapo amesimamia ufunguzi wa masoko mawili katika wilaya za Chunya na Mbeya.

Akiwa ziarani katika Wilaya ya Chunya Aprili 27, mwaka huu, Rais Magufuli alipata taarifa za Wilaya ya Chunya kuwa katika orodha ya wilaya zinazoongoza kwa utoroshaji wa dhahabu nchini, huku ikiwa bado haijatekeleza agizo la kufungua soko la madini hayo.

Baada ya taarifa hiyo alitoa siku saba kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Chalamila kuhakikisha soko hilo linafunguliwa, huku akisisitiza agizo hilo ndilo jaribu lake kubwa kwenye kibarua chake.

**Lengo lingine la kuanzisha masoko ya madini nchini ni kufanya mapato yatokanayo na tozo za uuzwaji wa madini hayo uwe wa wazi na kila mtu afahamu.**

Akizungumza jana jijini Mbeya wakati wa ufunguzi wa soko kuu la madini mkoani Mbeya, Chalamila alishukuru Wizara ya Madini na Tume ya Madini kwa ushirikiano walioutoa katika kufanikisha ufunguzi wa masoko hayo.

"Kama mnakumbuka rais Magufuli alitupa siku saba kuhakikisha tunafungua soko la dhahabu chunya, lakini pamoja na agizo hilo, ni utekelezaji wa sheria ya madini ili biashara ya uuzwaji na ununuzi wa madini yetu uwe wa wazi," alisema Chalamila.

Alisema lengo lingine la kuanzisha masoko ya madini nchini ni kufanya mapato yatokanayo na tozo za uuzwaji wa madini hayo uwe wa wazi na kila mtu afahamu.

Alisema Mei 2, mwaka huu walipokuwa wanazindua soko la madini wilayani Chunya, dhahabu iliyouzwa ilikuwa zaidi ta gramu 2,000 ambazo ziliuzwa Sh. milioni 174.9 na Serikali ikapata Sh. milioni 12.4. Alisema masoko hayo yanaongeza tija ya madini kwa wachimbaji, wanunuzi na Serikali kutokana na mfumo wa uuzwaji wa madini hayo kuwa wa wazi.

Mkurugenzi wa Ukaguzi na Biashara wa Tume ya Madini, Dk. Venance Mwasse, aliipongeza Serikali ya Mkoa wa Mbeya kuitikia agizo la serikali na kufungua masoko hayo haraka.

Alisema baada ya kufunguliwa kwa masoko hayo mawili mkoani Mbeya, yamefikia masoko 13 nchi nzima ambayo yameanza kufanya kazi na kwamba ufanisi wake unaonekana wazi.

Dk. Mwasse aliyataja maeneo mengine ambayo tayari masoko hayo yamefunguliwa ni Geita, Singida, Kahama, Arusha- Namanga, Ruvuma, Shinyanga na Katavi.

Mengine ni Dodoma, Tabora, Kigoma na Mara, na kwamba mikoa mingine ipo katika hatua za mwisho kukamilisha vigezo mbalimbali vikiwamo vya kiusalama na miundombinu.

"Katika soko hili kutakuwa na sehemu ya ukaguzi na uthaminishaji madini, kutakuwa na eneo la soko na kutakuwa na eneo ambalo miamala itafanyika na vibali vitatolewa, hivyo kutakuwa na huduma za Benki, TRA, Tume ya madini na Halmashauri," alisema Dk. Mwasse.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dar es Salaam, Kate Kamba (kushoto), akizungumza na wananchi wa Msakala, Kata ya Makangarawe, Wilaya ya Temeke, jijini juzi, akiwa katika ziara ya kuimarisha chama. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakulima wafurahia bei mahindi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa mahindi mkoani Mbeya, wameanza kufurahia kupanda kwa soko la zao hilo, huku baadhi wakiwa na wasiwasi wa kukumbwa na njaa kwa madai kuwa kupanda kwa soko hilo kunaweza kuchochea kuuza chakula chote.

Wakizungumza na Nipashe katika masoko mbalimbali baadhi ya wakulima, walidai licha ya sasa kuwa ni kipindi cha mavuno, lakini mahindi yanauzwa kuanzia Sh. 7,000 tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma. Geofrey Mwaigaga, alisema mwaka juzi kipindi kama hiki wanunuzi wa mahindi walikuwa wananunua kuanzia Sh. 3,000 mpaka 4,000.

Alisema kwa mwaka huu dalili za wakulima kunufaika na kilimo chao imeanza kuonekana na kwamba kuna taarifa kuwa baadhi ya mikoa kuna upungufu wa chakula kutokana na hali ya hewa, hivyo soko hilo linaweza kuendelea kupanda.

"Tunasikia baadhi ya mikoa kama Shinyanga kuwa hakuna mvua, lakini pia kule kwa wenzetu Kenye tunasikia watu wanakufa njaa, hivyo tunaamini kuwa kama soko limeanza hivi, kuna uwezekano likaendelea kuwa zuri zaidi," alisema Mwaigaga.

Jane Mogha, alisema kutokana na soko kuwa zuri, baadhi ya wakulima huwa wanashawishika na kuuza mavuno yote bila kubakiza akiba ya chakula, hivyo kusababisha njaa.

"Mwaka 2015 tulikuwa tunanunua mahindi mpaka Sh. 20,000 kwa debe kutokana na wakulima kuuza mazao yao mapema kwa wafanyabiashara waliokuwa wanatoka Kenya, sasa tunaomba mwaka huu isije ikafika huko," alisema Jane.





# Waomba marekebisho Sheria Kudhibiti Ukimwi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kufanyia marekebisho sheria ya kuzuia na kudhibiti ukimwi ya mwaka 2008 katika kifungu kikubwa cha 15 pamoja na kifungu kidogo cha 2, ili kiendane na wakati ulipo sasa.

Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Watoto nchini, Aidath Ishulula, wakati akizungumza na vyombo vya habari katika mkutano wa siku mbili ulioandaliwa na Shirika la Mtandao wa Watoto na Vijana Mwanza (MYCN).

Ishulula, alisema kuwa katika mkutano huo watoto pamoja na vijana walipata fursa ya kufanya mapitio katika sheria hiyo na kubaini kuwa vifungu hivyo vinatakiwa kufanyiwa marekebisho.

Alisema katika vifungu hivyo sheria hiyo inasema kuwa mtoto au mtu ambaye hana uwezo wa kupokea majibu ya upimaji wa VVU anaweza kupima kwa kupata ruhusa ya maandishi toka kwa mzazi au mlezi anayetambulika.

**Uganda sheria zao zinaruhusu kupima watoto katika umri huo hii itatusaidia kutambua afya zetu, lakini pia mtoto ni rahisi kupokea kitu tofauti na mtu mzima.**

Alisema kuwa kutokana na sheria hiyo kukataza mtoto chini ya miaka 18 kupima VVU imewanyima fursa wengi wao kutambua afya zao mapema.

Aidha, alisema serikali inatakiwa kufanya marekebisho ya sheria hiyo ili kuruhusu watoto kuanzia miaka 12 kupima bila kuwapo kwa ruhusa ya wazazi.

"Familia zetu nyingi hawana mwamuko wa kupima VVU, hivyo kutoa ruhusa kwa watoto kwenda kupima itakuwa ni changamoto tunaomba tupatiwe fursa hiyo kisheria katika umri huo wa miaka 12 kama ilivyo nchi nyingine," alisema.

Alifafanua kutokana na tafiti mbalimbali imebainika kuwa watoto wanaanza ngono katika umri wa kuanzia mika 10, hivyo itakua busara sheria hiyo kuwaruhu kupima VVU katika umri huo.

"Tunaomba kupima Ukimwi bila ruhusa ya wazazi katika umri wa miaka 12 hata nchi nyingine kama Rwanda, Uganda sheria zao zinaruhusu kupima watoto katika umri huo hii itatusaidia kutambua afya zetu, lakini pia mtoto ni rahisi kupokea kitu tofauti na mtu mzima," alisema.

Mwakilishi wa vijana, Mwinyi Halid, alisema kuwa kama serikali itafanyia marekebisho kifungu hicho itawawezesha kutambua afya zao mapema.

"Alisema kutokana na sheria kukataza watoto chini ya miaka 18 kupima mpaka wawe na ruhusa ya wazazi wao kumekuwa sababu ya watu kudanganya umri na kuchangia kuwapo kwa takwimu zisizo sahihi zinazohusu maambukizi ya VVU," alisema.

## Kalemani aagiza umeme upatikane mijini, vijijini Juni 30

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Medard Kalemani, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco) hadi kufikia Juni 30, mwaka huu, vijijini na mijini kuwe kumefikiwa na huduma ya umeme.

Waziri Kaleman aliyasema hayo katika ziara yake ya kikazi kwenye vijiji vya Ntyuka na Mkonze kwa ajili ya kukagua maeneo na nyumba ambazo hazina umeme.

Alisema hakuna sababu ya watu kutumia sola wakati uwezo wa kulipia ili waunganishiwe umeme wanao.

Hata hivyo, aliwataka Tanesco kuacha tabia ya kukataa kupokea fedha kutoka kwa wateja ili wawekewe nguzo kwa ajili ya kupata huduma za umeme na badala yake wametakiwa kupokea ili kuweka kila eneo.

Alisema kinachotakiwa ni kupokea hela na kuwawekea nguzo, hakuna haja ya kukwepa kazi wanazowapa wananchi. Kalemani alisema wananchi jijini Dodoma wameelimika kutokana na kujenga nyumba bora ambazo zinastahili kuwa na umeme.

Alifafanua kuwa endapo watashindwa kutekeleza huduma hiyo ya uwekaji umeme, hatua kali dhidi ya mameneja zitachukiliwa.

"Meneja nakuomba utekeleze hili agizo usipofanya hivyo hatua kali zitachukuliwa dhidi yako," alisema Kalemani.

Alisema lengo lake ni kuona nchi nzima watu wanatumia umeme badala ya sola kama ilivyo katika baadhi ya vijiji.

Alisema Dodoma ni jiji kwa hiyo linapaswa kuwa na umeme kila pembe ili hadhi ya jiji ionekane.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kutandaza nyaya wakati wakisubiri kuwekewa umeme ikiwamo kwenda kuomba huduma hiyo tayari kwa kuunganishwa.




Spika wa Bunge, Job Ndugai (wa pili kulia), akikabidhiwa msaada wa mifuko 530 ya saruji yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 10 na Kaimu Mkurungenzi wa Masoko na Huduma wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), Elisante Maleko (wa pili kushoto), kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Shule ya Msingi Karume, Wilaya ya Kongwa, mkoani Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ndugai azitaka kamati shule kutoa taarifa mapato, matumizi

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

SPIKA wa Bunge Job Ndugai, amezitaka kamati za shule na ujenzi kutoa taarifa za mapato na matumizi kwa wananchi kwa wakati ili kuondoa malalamiko.

Alitoa agizo hilo wakati alipokuwa akipokea msaada wa mifuko ya saruji 530, kutoka Shirika la Bima ya Taifa (NIC), katika Shule ya Msingi Karume, mji mdogo wa Kibaigwa.

Ndugai alisema kamati za shule zinatakiwa kutoa taarifa za mapato na matumizi kwa wakati kwa wananchi, ili kuondoa malalamiko yanayojitokeza.

"Kuna wakati mwingine wananchi wanashindwa kutoa michango mbalimbali kwa ajili ya maendeleo kutokana na kutokuwapo kwa uwazi wa michango waliyotoa, kwa njia hiyo mnawavunja moyo wananchi kuchangia," alisema.

Alisema kamati hizo zinatakiwa kuwajibika kutoa hesabu za michango mbalimbali wanayotoa kabla ya kuagiza mingine.

Aidha, alisema mji huo wa Kibaigwa unahitaji shule zingine sita ili kukabiliana na ongezeko kubwa la watoto katika eneo hilo.

Alisema kwa sasa shule zilizopo zinawastani wa watoto 200 kwa kila darasa hivyo miundombinu ya majengo na matundu ya vyoo inahitajika haraka.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Karume wilayani Kongwa, Gardson Mwalukasa, alisema shule hiyo inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa pamoja na madawati.

Aliitaja changamoto nyingine kuwa ni upungufu wa nyumba za walimu pamoja na matundu ya vyoo.

Changamoto nyingine aliijata kuwa ni kelele za magari na pikipiki zinazotokana na gereji zilizopo jirani na maeneo ya shule na mapito holela ya wananchi katika eneo la shule.

Mwalukasa alisema kwa sasa shule hiyo ina idadi ya wanafunzi 2,144 na hivyo kutokana na idadi hiyo shule inakabiliwa na changamoto hizo.

Kwa upande wake Kaimu Mkurungenzi wa masoko na huduma kwa wateja wa Shirika la Bima la Taifa, Elisante Maleko, alisema shirika hilo limekabidhi msaada huo wa mifuko 530 ya saruji ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Dk. John Magufuli, katika elimu.

Alitaja thamani ya msaada wa mifuko hiyo kuwa ni zaidi ya Sh. milioni 10, ikiwa na lengo la kurudishia wananchi sehemu ya faida wanayoipata.

Aidha, alisema shirika hilo linamilikiwa na serikali kwa asilimia 100 hivyo faida inayopatikana inarudishwa kwa wananchi ili kuunga mkono serikali katika kuwahudumia watu wake.

Aliwashauri wananchi kukata bima za mali zao za maisha ili kuwakinga wakati wa majanga mbalimbali wasibaki kulalamika wakati wa matatizo yakiwafika.

Katika mkutano wa makabidhiano iliendeshwa harambee ndogo na kupatikana mifuko ya saruji 233 pamoja na Sh. 2,645,900.





# Makamu wa Rais asisitiza umuhimu wa kujua historia

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema wananchi wanapaswa kujua historia yao katika dhana nzima ya kuendelea kulinda uhuru wao, heshima, utamaduni na hata mazingira yao yanayowazunguka.

Alisema binadamu asiyejua historia yake kamwe anakuwa mtumwa (kibaraka), wakati wote akiendelea kutawaliwa kifikra jambo ambalo ni hatari katika maisha yake yanayomuhusu.

Balozi Iddi alisema hayo alipofanya ziara ya kuyakagua mahandaki mawili ya Manga, Pwani yaliyokuwa yakitumika kuhifadhia watumwa ambayo kwa sasa yamekuwa sehemu muhimu ya kujifunza historia ya biashara hiyo iliyopigwa marufuku tokea karne ya 18.

Alisema Zanzibar ilikuwa kituo muhimu cha historia iliyounganisha sehemu nyingi duniani, historia ambayo taasisi inayosimamia masuala hayo ambayo ni Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale ina jukumu la kusimamia vyema maeneo yote muhimu ili wageni pamoja na wananchi wapate fursa ya kujifunza zaidi.

**Mpango huo umeanza kufanya kazi kwa kuwahusisha watendaji wa wizara hiyo kama mwelekeo wa kuhamasisha ili kuungwa mkono ya wizara nyengine na baadaye wananchi.**

Aliwataka vijana wanaosimamia maeneo hayo kufanya jitihada ya kujifunza historia kamili ili kuepuka tabia ya kutoa taarifa zisizo na uhakika za maeneo wanayofanyia kazi.

Akitoa ufafanuzi, Msimamizi wa Mahandaki hayo Makame Omar Said, alisema maumbile ya eneo hilo muda wote yamekuwa ya kujificha kutokana na hali halisi ya biashara yenyewe ya utumwa ilivyokuwa ikifanywa kwa kujificha.

Makame alisema utafiti unaonyesha wazi kwamba bado idadi ya wazawa kufika eneo hilo kwa ajili ya kujifunza historia yake ni ndogo ikilinganishwa na wageni pamoja na wasomi wa fani za kihistoria.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Khadija Bakari Juma, alisema wizara hiyo kwa sasa tayari imeshaandaa mpango maalum wa kuhamasisha utalii wa ndani ili kuimarisha zaidi mapato ya taifa.

Khadija alisema mpango huo umeanza kufanya kazi kwa kuwahusisha watendaji wa wizara hiyo kama mwelekeo wa kuhamasisha ili kuungwa mkono ya wizara nyengine na baadaye wananchi.

Aliishukuru Serikali ya Zanzibar kwa uamuzi wake wa kutenga bajeti maalum kila mwaka inayolenga kuhudumia uhifadhi wa maeneo ya kihistoria jambo ambalo limeleta matokeo mazuri katika usimamizi wa maeneo hayo muhimu.

Akielezea changamoto zinayoyakabili maeneo mengi ya kihistoria Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "B" Rajab Ali Rajab, alisema kwamba uhaba wa wafanyakazi ni tatizo kubwa linalofaa kuangaliwa na serikali pamoja na taasisi inayosimamia maeneo hayo.

Rajab alisema ufinyu huo wakati mwengine hutoa mwanya kwa wahalifu kufanya hujuma katika maeneo hayo ambayo kwa namna yoyote ile yanapaswa kuheshimiwa na kuenziwa kwa vizazi vya sasa na vile vijavyo.

## Vijana watakiwa kuwa wazalendo kwa kufanyakazi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Wizara ya Kazi Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Moudline Castico, amewataka vijana kuwa wazalendo kwa kufanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo waliyojiwekea.

Aliyasema hayo kwa niaba ya Rais wa Zanzibar katika uzinduzi wa ushirika wa Mwangaza wa kijani pamoja na kampuni ya Broadway limited huko katika viwanja vya Kariakoo mjini Unguja.

Alisema vijana wanapaswa kuungwa mkono juhudi zao ili waweze kufikia malengo ya kuanzishwa kwa vikundi au ushirika katika maeneo yao ikiwamo kujiendeleza katika harakati za kimaisha.

Alisema ushirika unasaidia kwa kiasi kikubwa katika kuwapatia vijana ajira ikiwamo hata kujiajiri wao wenyewe kupitia shughuli zao mbalimbali wanazozifanya.

Alisema vikundi vya ushirika vinasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza wimbi la vijana wanaojihusisha na vitendo viovu na hata vitendo vya udhalilishaji kwa visingizio kwa kutokuwa na ajira na kushindwa kujiajiri.

"Ushirika ni njia ya kuwakutanisha vijana kwa pamoja na kufanya kazi zao kwa bidii, hivyo ushirika huu nataka usonge mbele zaidi kwa kuwa na wanachama ambao watahakikisha ushirika unasimama na hata kuanzisha miradi mbalimbali," alisema.

Aidha, aliutaka ushirika huo kufanya kazi kwa ushirikiano ili kufikia lengo la kuanzishwa kwake ikiwamo kutofanya kazi kwa mazoea.

Aliutaka ushirika huo kutojihusisha na masuala ya udhalilishaji wa kijinsia na badala yake wawe mstari wa mbele katika kukemea vitendo hivyo ambavyo vinatia aibu katika jamii ya kizanzibar na nchi kwa ujumla.

Wakisoma risala yao mmoja wa wanachama wa ushirika huo Sharifa Haji, alisema changamoto kubwa inayoukabili ushirika wao ni kutokuwa na ofisi kubwa yenye nafasi kwaajili ya kufanyia shughuli zao pamoja na shamba kuendesha shughuli za kilimo.

Alisema ofisi waliyo nayo sasa haitoshi kulingana na idadi ya wanachama waliopo hivyo kusababisha kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, Luiza Mlelwa, akizungumza kwenye mkutano wa mwaka wa Chama cha Ushirika cha Msingi Umoja, uliofanyika wilayani humo, mkoani Lindi juzi. Wengine ni viongozi wa chama hicho.
PICHA: SABATO KASIKA

# Spika ahimiza uchangiaji damu mara kwa mara

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid, amesema jamii ikiendelea kuwa na mwamko wa uchangiaji damu mara kwa mara, itasaidia kupunguza idadi ya vifo vya wajawazito wanaojifungua na kufariki kutokana na upungufu wa damu mwilini.

Akizungumza katika bonaza la uchangiaji damu lililofanyika viwanja vya Maisara mjini Unguja, alisema uchangiaji wa damu hauna dini, wala chama cha siasa, bali jamii inatakiwa kuunga mkono, ili benki ya damu iweze kukusanya uniti nyingi za damu na kuigawa kwa jamii.

Alisema jamii lazima ijenge utamaduni wa kuchangia damu mara kwa mara ili kupunguza upungufu uliopo katika benki ya damu na hospitali mbalimbali za Zanzibar na hatimae kuokoa maisha ya wagonjwa wanaofika hospitali.

Spika Zuber aliwapongeza viongozi wa halmashauri, Manispaa na Wilaya wa Zanzibar kwa kuthamini na kuunga mkono jitihada zinazochukuliwa na wananchi katika suala zima la uchangiaji damu.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, alisema hakuna saba bu ya chupa 1,500 zinazohitajika katika benki ya damu kutopatikana kutokana na mwamko na uungwaji mkono mkubwa uliojitokeza kwa wananchi wa mkoa huo.

Alisema serikali ya mkoa huo inathamini upendo na mshikamano unaoonyeshwa na wananchi wa mkoa huo kwa kupokea maagizo na maelekezo ya serikali hususani katika suala la uchangiaji damu kwa kuwa ni la kiimani zaidi.

Kwa upande wake, Meneja Mawasiliano kitengo cha damu salama, Bakari Hamad Magarawa, alisema wananchi wakumbuke kuwa damu haiuzwi, hivyo jukumu lao ni kuchangia na kuwataka kuripoti mwananchi anapotakiwa kuuziwa damu.

Katika uchangiaji damu zaidi ya chupa 1000 zilipatikana itakayoiwezesha benki ya damu kuwa na akiba.

**HABARI KITAIFA**

# Miwa yawaletea fursa Chamwino

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ametangaza eneo la Dabalo Wilaya ya Chamwino Mkoa wa Dodoma, kuwa Mji Mdogo na kuagiza wamiliki wa ardhi katika eneo hilo kupimiwa na kupatiwa hati ya umiliki wa ardhi.

Lukuvi alitangaza eneo hilo jana katika Kata ya Dabalo wilaya ya Chamwino Mkoa wa Dodoma wakati wa kumtangaza mwekezaji kiwanda cha sukari kampuni ya Purandare Industries Ltd ya India kupatiwa eneo kwa ajili ya uzalishaji sukari.

**Kutokana na eneo hilo kupangwa kimji, sasa maeneo ya mji huo yatamilikishwa kwa hati ya miaka 99.**

Lukuvi alisema ametangaza eneo hilo kuwa mji mdogo kutokana na mamlaka aliyopewa na kubainisha kuwa kuanzia sasa ardhi ya mji huo haitasimamiwa tena na serikali ya kijiji bali itakuwa eneo la kimji na ardhi yake kupangwa kama ile ya Dodoma mjini.

Waziri Lukuvi alisema kutokana na eneo hilo kupangwa kimji, sasa maeneo ya mji huo yatamilikishwa kwa hati ya miaka 99 na utoaji hati za kimila hautafanyika tena na kusisitiza kuwa wananchi wa Dabalo watakaopimiwa hawatatozwa tozo kubwa kama wanavyotozwa wananchi wa maeneo mengine.

Kuhusu mwekezaji kumilikishwa eneo la uwekezaji kwa ajili ya uanzishaji kiwanda cha kuzalisha sukari, Lukuvi alisema taratibu zote za kumuwezesha mwekezaji huyo kuanza uzalishaji zimekamilika ikiwamo cheti kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na ile ya Mazingira kupitia Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na kusisitiza kuwa anataka eneo la Dabalo liwe mji wa sukari.

Kwa mujibu wa Lukuvi, Mwekezaji huyo kutoka India atakuwa na jukumu la kununua sukari ya wakulima katika eneo la Dabalo, kusaidia wakulima kulima zao sambamba na kuboresha miundombinu katika eneo hilo.

Kwa upande wake Mwekezaji Purandare Industries Ltd, Satish Purandare, aliahidi kuleta vifaa ikiwamo matrekta katika kipindi cha miezi miwili kwa ajili ya kusaidia ulimaji zao la miwa na uzalishaji wake kuanza mapema mwakani na kuongeza kuwa kampuni yake itaajiri wafanyakazi kutoka kijiji cha Dabalo na kwa zile kazi za kitaalamu watakaopewa kipaumbele ni Watanzania.

Tangu Rais John Magufuli aeleze Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na TIC kuchelewesha kutoa vibali kwa mwekezaji sukari nchini na kutoa wiki moja kwa Wizara na TIC kushughulikia suala, tayari ndani ya wiki mbili Lukuvi amewezesha wawekezaji wawili wa sukari katika eneo la Mvua Morogoro Vijijini na Dabalo Chamwino Mkoa wa Dodoma kuwekeza ambapo wote kwa pamoja watakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 94,000 za sukari kwa mwaka.




Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kukagua maeneo ambayo hayajaunganishwa na umeme katika eneo la Mkonze, jijini Dodoma juzi. Wengine ni Watendaji wa Shirika la Umeme la TANESCO na Wizara ya Nishati. **PICHA: WN**

# Ajali za barabarani bado tishio

**Na Mary Geofrey**

WATU 29 wanapoteza maisha kati ya ajali 100,000 zinazotokea kwa sababu mbalimbali nchini, kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) za mwaka huu.

Licha ya juhudi mbalimbali zinazofanywa za kupunguza vifo hivyo, takwimu zitokanazo na ajali zinaongezeka kidunia kutoka watu milioni 1.2 waliopoteza maisha miaka ya nyuma hadi watu milioni 1.3.

Hayo yameelezwa na Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kitengo cha Usalama, Mary Kesi, wakati akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu maadhimisho ya wiki ya usalama barabarani Kimataifa, inayoanza leo had Mei 12 mwaka huu, yenye kauli mbiu inayosema 'Uongozi mahiri kwa usalama barabarani, paza sauti, okoa maisha'.

Alisema nchini wastani uliowekwa wa vifo vya ajali za barabarani ni asilimia 26 kati ya ajali 100,00, Afrika asilimia 18 kati ya ajali 100,000, Ulaya asilimia tisa kati ya ajali 100,000 na kidunia asilimia 18 kati ya ajali 100,000.

"Kunzia kesho (leo), tunaanza wiki ya Usalama Barabarani Kimataifa na kuna makubaliano ya mpango kazi wa dunia wa miaka 10 ya kupunguza ajali za barabarani kufika nusu. Licha ya juhudi zinazoendelea kufanywa na wadau mbalimbali bado idadi ya wanaototeza maisha ni kubwa kulinganisha na takwimu zilizowekwa," alisema.

Alisema nchini kwa mwaka 2018 watu 32 walipoteza maisha katika ajali 100,000 zilizotokea, mwaka huu watu 29 kati ya ajali 100,000 na madereva wa bodaboda wanaongoza kwa asilimia 28 na watembea kwa miguu kwa asilimia 26.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (Tawla), Mary Richard, aliitaka Serikali kusimamia maboresho ya sheria za usalama barabarani katika kupunguza janga hilo.

Alisema sheria ya usalama barabarani iliyopo sasa inamtambua dereva wa pikipiki ndiye anapaswa kuvaa kofia, haimzungumzii abiria, pia inazungumzia dereva na abiria wa mbele wanapaswa kufunga mkanda lakini haiwazungumzii abira wa nyuma.

Alisema pia sheria haimzungumzii mtoto ambaye anapaswa kuwa na kiti chake kwa ajili ya kumlinda wakati wa ajali.

"Taasisi za kiraia ambazo zimekuwa zikisimamia usalama batabarani tunaishinikiza Serikali kusimamia mabadiliko ya sheria ili kusaidia kupunguza vifo vya watu wanaopoteza maisha kila siku kutokana na ajali," alisema.

# Takwimu sahihi za chakula zatakiwa

**Na George Tarimo,** IRINGA

MAMLAKA ya Uendelezaji Biashara (Tantrade), imewataka maofisa biashara wa Halmashauri na mikoa pamoja na maofisa kilimo kuwa na takwimu sahihi za chakula kinachovunwa katika maeneo yao ili kuiwezesha mamlaka hiyo kuwa na takwimu sahihi za ziada iliyopo kwa ajili ya kuitafutia soko ndani na nje.

Kauli hiyo imetolewa Mjini Iringa na Mkurugenzi Mkuu wa Tantrade, Edwin Rutageruka, kwenye mkutano wa wadau wa nafaka ambapo amesema kukosekana kwa takwimu sahihi za mazao ya chakula yanayovunwa imekuwa ni changamoto katika kutafuta masoko ya mazao hayo inapopatikana ziada.

Rutageruka alisema kuna ofisa ya biashara, mrajisi, kilimo lakini katika tathmini wamebaini kila mmoja ana taarifa zake na baadhi yao kila mmoja anaona haki ya kuwa na taarifa hizo mfukoni wakati mwenzake hana, hivyo kuna haja kila mmoja kwa na mtandao mmoja wa kushirikiana na kuongea lugha moja.

Rutageruka alisema utafiti wao walioufanya hivi karibuni wamebaini baadhi ya mazao kutokuwa na ubora wa mazao, kutokuwa na takwimu na ubora wa ziada ya mazao ya chakula, wakulima na wafanyabiashara kutokuwa waaminifu kwa kutokutoa taarifa kamili za mazao na uelewa duni wa vyama vya ushirika.

Nyingine ni kutokuwa na uelewa wa mfumo wa stakabadhi ghalani, hivyo kubaki kunyonywa na madalali, baadhi ya mikoa na halmashauri kutokuwa na takwimu sahihi ya ziada ya mazao yaliyopo ghalani.

Naye Endmond Ntiba, ofisa kilimo kutoka idara ya maendeleo ya mazao Wizara ya Kilimo, alisema pamoja na uwezo wa wakulima kuzalisha chakula na ziada ambayo huuza ili kujipatia kipato, wizara inalo jukumu la kufanya utafiti wa haraka ili kujihakikishia usalama wa chakula na pia kudhibiti mfumuko wa bei.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, akitia saini katika kitabu cha maombolezo ya Msiba wa aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, nyumbani kwa Marehemu Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: UTUMISHI**

# Pinda ashauri wasomi kubadili elimu ya darasani

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amesema ipo haja kwa wasomi nchini kuangalia namna ya kuibadilisha elimu ya darasani ili iweze kuendana na uhalisia wa maisha katika kutatua changamoto halisi za jamii.

Akizindua wiki ya tano ya utafiti iliyoanza jana katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Pinda alisema kumekuwa na mjadala duniani kuhusu elimu inayotolewa na mbinu zinazotumika kufundishia hasa kwa nchi zinazoendelea.

Alisema vyuo vingi duniani hasa katika nchi zinazoendelea baada ya kubaini kuwa elimu ya darasani isiyo na uwiano na uhalisia wa kimaisha ina matatizo, vimeamua kufuata mfumo wa elimu ya juu ambao unalenga kuingiza masuala ya ubunifu na ujasiriamali katika mitaala ya masomo.

Aidha, alisema elimu hiyo inatumia utatuzi wa changamoto halisi zilizopo katika jamii kama njia ya kuhuisha, huku akiwataka UDSM kuongeza kasi ya ufundishaji wa vitendo kwa kuwa ndiyo njia pekee itakayosaidia chuo hicho kwenda na wakati na kutambulika kitaifa na kimataifa.

"Chuo sasa kitaweza kuzalisha wahitimu bora ambao wataweza kutoa mchango mzuri zaidi katika jamii na maendeleo ya utafiti kwa jamii, wahitimu watatumia ujuzi na maarifa waliyoyapata kwa kujiajiri na kuajiri vijana wenzao au kuajirika katika fani mbalimbali kwa urahisi," alisema.

Pinda aliyekuwa Waziri Mkuu wa serikali ya awamu ya nne, alisema miradi ya utafiti inaongeza thamani kwa miradi ya maendeleo na vipaumbele vya nchi hasa wakati huu wa uchumi wa viwanda.

"Utafiti unaofanywa na watafiti wetu ulenge kukidhi mahitaji ya taifa ya utafiti na ubunifu. Tunaomba watafiti wote waliopata ruzuku ya utafiti wa UDSM watumie fedha vizuri na kufanya utafiti utakaoleta matokeo chanya kwa jamii kwa kuzingatia malengo na muda uliopangwa," alisema.

Aidha, alisema uamuzi wa chuo kutenga fedha kwa ajili ya utafiti, utatoa fursa nyingi iwapo watajipanga kuboresha sera, kuhuhisha miundombinu ya utafiti na ubunifu, kupangilia na kusimamia vizuri raslimali zilizopo na kubadili baadhi ya desturi za kitaaluma ambazo zimepitwa na wakati.

"Miaka ya 1980 hadi 90 UDSM ilikuwa na taasisi za ubunifu na utafiti ambazo zilifanya kazi kubwa ambazo pamoja na kutatua changamoto na kuchangia katika maendeleo ya nchi zilikiletea chuo heshima kubwa. Mfano ni taasisi ya bidhaa za ubunifu ambayo ilijikita kubuni na kusambaza teknolojia zilizotumiwa na wananchi katika shughuli za uzalishaji," alisema.

Kwa mujibu wa Pinda, kipindi hicho kilikuwa ni kigumu cha uchumi wa nchi kutokana na uhaba wa bidhaa mbalimbali kama sabuni, mafuta ya kupitia na sukari, lakini taasisi hiyo ilibuni teknolojia na kutengeneza mashine ambazo zilitumiwa moja kwa moja na wananchi hasa vijijini kwa malighafi walizozalisha wenyewe.

Awali, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Willium Anangisye, alisema ili kuwe na maendeleo ya ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla utafiti ni muhimu katika ngazi ya jamii na uwasilishaji wa matokeo kwa wadau wakiwamo wanataaluma, watunga sera, wafanyabiashara na wenye viwanda.

Alisema kupitia utafiti ndipo watu watafanya maamuzi mazuri na sahihi kwa maendeleo ya taifa na binadamu kwa ujumla, na katika ngazi ya chuo unasaidia kukitangaza na kuimarisha uhusiano wa kimataifa na chuo hicho kimekuwa mfano ndani na nje ya nchi.

# Wenye matatizo ya magoti, nyonga kufanyiwa uchunguzi

**Na Mwandishi Wetu**

DAKTARI bingwa wa upasuaji wa nyonga na magoti kutoka India, Dk. Yuvraj Lakum, anatarajiwa kuwafanyia uchunguzi na upasuaji watu wenye matatizo hayo nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na hospitali ya Regency, uchunguzi wa magonjwa hayo utafanyika kuanzia tarehe 9,10 na 11 mwezi huu katika hospitali hiyo Upanga jijini Dar es Salaam.

Ilisema ujio wa mtaalamu huyo utapunguza gharama za wagonjwa kwenda nje ya nchi kufuata tiba hiyo.

"Katika jitihada za kupunguza rufaa za wagonjwa kwenda matibabu nje ya nchi na kuokoa fedha nyingi za kigeni ambazo zimekuwa zikitumika tumeona ni vyema kuita mara kwa mara mtaalamu huyu kufanya upasuaji hapa Dar," ilisema taarifa hiyo.

Ilisema ujio wa mtaalamu huyo umekuwa ukisaidia kuwapa ujuzi wataalamu wa ndani ili mwishowe wawe na utaalamu wa kufanya upasuaji wa aina hiyo wao wenyewe.

Aidha, ilisema mpango wa kuita madaktari hao bingwa wa magoti na nyonga umekuwa ukiratibiwa na hospitali ya Regency kwa kushirikiana na hospitali ya HCG Multi-Specialty iliyoko mji wa Ahmedabad nchini India.

"Tunatarajia mtaalamu huyo atafanya uchunguzi kuanzia tarehe nane Juni hadi tarehe 10 na wale watakaobainika kuwa na matatizo hayo watafanyiwa upasuaji baada ya wiki sita," alisema.

" Hii ni fursa ya kipekee kwa Watanzania wenye matatizo kama haya kuchangamkia fursa hii kwani badala ya kwenda nje na kutumia gharama kubwa kusafiri na wasaidizi wao kwenda nje ya nchi sasa wanafanyiwa upasuaji hapa hapa nchini," ilisema taarifa hiyo.




## TANGAZO


absa
It takes a solid foundation to make it to the Top 40 Index on Africa's leading stock exchange.
Whether it's taking your business places, growing your wealth or building a legacy, we are a well-capitalised organisation with the global reach to help get you there.
As one of the largest companies listed on the Top 40 Index on the Johannesburg Stock Exchange, we have a market capitalisation of over US$12 billion (as at 31 December 2017), and a balance sheet of over US$97 billion in assets, enabling us to deliver the best solutions for our varied client portfolio.
www.absa.africa
Absa Group, proudly serving you as Barclays in Tanzania.
BARCLAYS
© Absa Group Limited Reg No 1986/003934/06. All rights reserved

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.
Baruapepe: ceo@kses.co.tz.


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JULIUS FAUSTINE SHIRIMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T. 460 BTH. TOYOTA.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MB/RB/3907/2019.**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA KINONDONI**
**KINONDONI**
**MIRATHI NA 08 YA 2019**
**Maombi ya barua ya Usimamizi wa Mirathi ya Marehemu PETER JOHN MOSHA**
**NA**
**HYASINTA PETER MOSHA..........WAOMBAJI/MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na Haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia Mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji hapo juu
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 29 mwezi 05, mwaka 2019.

Imewasilishwa......................Leo tarehe 03 mwezi 05, mwaka 2019.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA KIVUKONI/KINONDONI

215214902

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LUCY JOSEPH KAINGILILA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TRACTOR yenye namba za usajili T752DHP. Chassis namba MEA35E65YG1100155. Engine namba S433A80252.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KNG/RB/678/2019**

115214702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MWANZA**
**SHAURI LA MADAI YA ARDHI NAMBA 85 YA 2018**
**SAFIA ALLY KOPESHA..................... MDAI**
**DHIDI YA**

1. ABDALLAH ALLY
2. MAGDALENA ZABRON............WADAIWA

**KUITWA SHAURINI**

KWA 1.ABDALLAH ALLY
2. MAGDALENA ZABRON
POPOTE MLIPO

Mnajulishwa kuwa shauri la madai tajwa hapo juu lilifunguliwa katika mahakama hii na limepangwa tarehe 07/05/2019 saa 3:00 asubuhi
Hivyo mnaamriwa kufika mahakamani muda na siku iliyopangwa bila kukosa. Endapo hamtahudhuria mahakamani, mtambue kwamba shauri hili litasikilizwa na kuamriwa bila ninyi kuwepo.
Imetolewa kwa AMRI na LAKIRI ya Mahakama hii leo tarehe 03/05/2019

115213802

### KUPOTELEWA NA LISTI

**KOLONEL MABULA BENEDICTO**
Anatanagza kupotelewa na listi za kulipia kodi ya kiwanja kitaro L (HD) 79 za mwaka 2017 kilichopo Malunga kiwandani katika Wilaya ya kahama,hati ya mauziano ya kiwanja kitaroL (HD) 79 na hati ya mauziano ya Bw. Marco Bundala na Alex Donard Mageni na hati ya mauziano ya bwa. Alex Donard Mageni na Koloniel Mabula Benedicto ya kiwanja kitaro L(HD) 79.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa katika kituo cha polisi kilichopo karibu yake Au piga simu namba;

0682-878-487 / 0743- 177-040.
Taarifa ya Polisi. KAH/RB/1892/2018.

115213902

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**VIVIENNE BRENNAN BRENNAN A**NATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI
YENYE NO T116 ATF SUZUKI ESCUDO. ENGINE NO G16A253774. CHASSES S NO TDOIW117143.

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.
**AR/RB/4813/019.**

115214002


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la*

*Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

TANGAZO

TCC



**The Board of Directors,**
**Management and Staff** of **Tanzania Cigarette**
**Public Limited Company** (TCC Plc)
are deeply saddened with the passing of Dr. Reginald Mengi.

The late Dr. Mengi was a key figure in driving industrialization in the private sector in Tanzania. His legacy as a Leader, Visionary and Philanthropist has left a mark for future generations.

**Our heartfelt condolences to his family, IPP Group and all Tanzanians.**

May God rest his Spirit in Eternal Peace.

**Amen**

# PJANIC AFIKIRIA KWENDA PSG




**ROME,** Italia

MIRALEM Pjanic amezungumzia kuhusu majaliwa yake hapo Juventus huku akifikiria uhamisho wa kuhamia kwa miamba wa Ufaransa, Paris Saint-Germain.

Akizungumza na televisheni ya Canal+, kiungo Pjanic amesema alivutiwa na PSG ambapo atakuwa tayari kusilikiza ofa yao.

"Paris ni moja ya klabu kubwa nane Ulaya kwa wakati huu, na kwa namna fulani kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wanataka kwenda mbele zaidi kuliko walivyofanya hivi karibuni," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29.

"Kuna klabu kubwa na klabu ambazo kila mchezaji yupo tayari kwenda kwa sababu wana miradi mizuri ya michezo na wachezaji wakubwa wanakwenda pale. Unakuwa na nafasi ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya pale.

"Kuna klabu kubwa ambazo zinawaheshimu wachezaji na wanawasikiliza. Pjanic ametumia misimu nane akiwa nchini Italia, kwa mara ya kwanza akiwa na AS Roma halafu akajiunga na Juve mwaka 2016, ambako ameshinda mataji ya Serie A mara tatu.

Aliongeza mkataba wake hadi mwaka 2023 mwaka jana, lakini hajaondoa uwezekano wa kuondoka kipindi cha majira ya joto.

"Kila kitu kinawezekana kwenye soka," alisema. "Nimekuwa nchini Italia kwa miezi nane kwa sasa, na kwa kweli nipo kwenye klabu kubwa hapa Juventus. "Kwenye soka kamwe huwezi kujua nini kitatokea. Kama kila mmoja yupo kwenye makubaliano, tunaweza kuzungumzia kuhusu kuondoka.

"Nifikiri kuhusu kumaliza msimu wangu, malengo yangu ni kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa miaka michache ijayo."

# *Cahill amtolea uvivu Sarri*




**LONDON,** England

NAHODHA wa Chelsea, Gary Cahill ameanzisha mashambulizi kwa kocha, Maurizio Sarri, akisema kwamba alijaribu kumuonyesha heshima kocha huyo ambaye amemweka benchi pale Stamford Bridge.

Sarri alisema hadharani kwamba Cahill hana mbinu za kutosha kuweza kucheza soka na kumfanya beki huyo kutoanza kwenye mchezo wowote wa mashindano yote tangu Novemba mwaka jana na amecheza mechi nne tu tangu hapo.

Cahill mwenye umri wa miaka 33, ameliambia gazeti la Daily Telegraph jinsi Sarri anavyomfanyia imemfanya kutokuwa na furaha dhidi ya kocha huyo raia wa Italia.

"Imekuwa hali ya kutisha kwa upande wangu," amesema Cahill ambaye huu ndio msimu wake wa mwisho hapo Chelsea, kwani mkataba wake unamalizika kipindi hiki cha majira ya joto.

"Kila kitu kitafutika kichwani mwangu wakati nitakapoondoka Chelsea. Kumbukumbu ya mwisho itakuwa ni fainali ya Kombe la FA tuliposhinda bao 1-0 dhidi ya Manchester United.

"Umekuwa ni wakati mgumu kwangu. Nimekuwa nikicheza mara kwa mara kwa kipindi cha misimu sita iliyopita na nimeshinda kila kitu nikiwa na Chelsea.

"Lakini sasa nilikuwa naangalia mechi nikiwa jukwaani, sikutarajia kitu kama hicho. Najua jinsi klabu zote zinavyofanya kazi, nina mahusiano mazuri na wachezaji wote pamoja na benchi la ufundi, na bado sijapewa nafasi niliyotarajia."

## Dembele kuikosa Liver leo

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imesema kuwa mshambuliaji wa kimataifa wa Ufaransa, Ousmane Dembele, ameumia mguu na hatakuwa fiti kucheza mchezo wa leo wa hatua ya nusu fainali ya pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool.

Mabingwa hao wa Hispania walithibitisha Jumapili kuwa uchunguzi unaonyesha kwamba Dembele aliumia misuli ya nyama za paja kwenye mchezo wa Jumamosi dhidi ya Celta Vigo ambao walifungwa 2-0.

Barcelona haikusema ni muda gani wanatarajia kumkosa mchezaji huyo, lakini hatakuwa katika kikosi kitakachoivaa Liverpool kwenye dimba la Anfield leo Jumanne, ambapo miamba hao wa Katalunya watakuwa wakilinda ushindi wao wa mabao 3-0 walioupata nyumbani kwao.

Hii ni mara ya tano kwa Dembele kuumia tangu alipojunga na Barcelona mwaka 2017.

Dembele mwenye umri wa miaka 21, amefunga mabao 14 katika mechi 42 alizoichezea Barcelona msimu huu.

Barcelona tayari imetwaa ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, lakini pia itacheza fainali na Valencia kwenye mechi ya Kombe la Copa del Rey Mei 25 mwaka huu.



## HABARI MICHEZO

# ...ONDOO ZA SOKA ...AGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER: SIWEZI KUSEMA CHOCHOTE

### Ni kuhusu hatima ya nyota wa United baada ya kushindwa kumaliza katika...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema kuwa timu yake ipo sehemu ambayo inastahili kuwapo.

**United haina budi kucheza Ligi ya Europa msimu ujao baada ya Huddersfield kudidimiza nafasi yao ya kumaliza kwenye "Top Four" ya Ligi Kuu England.**

"Katika kipindi cha muda mrefu, hatujawahi kuwa na changamoto kubwa katika Ligi ya Mabingwa Ulaya, na leo (juzi), tumeishi na matumaini ya mwisho yanayoondolewa, hivyo sio kitu kilichokuja kwa mshangao.

"Tulitarajia kushinda mchezo na kuonyesha ubora wetu, Manchester United bado haijawa vizuri kuwa na ushindani katika Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Siwezi kuzungumza juu ya watu sasa, lakini kuna fursa umeona mwisho wa wachezaji," alisema Solskjaer.

"Kwa sasa siwezi kusema lolote kuhusu yeyote , sidhani hiyo ni haki. Tumekuwa tukifukuzia pointi tatu katika kila mchezo.

"Lakini hatupaswi kuzungumza juu ya nafasi ya nne kwa Manchester United. Ni msimu mpya wa msimu ujao, tunahitaji kwenda kupambana kweli kwa sababu tunataka kurudi kwenye nafasi yetu ya nne juu.

"Sisi tuko katika ngazi nyingine baada ya kutoka Liverpool na Manchester City, lakini hiyo ni ukubwa wa changamoto na ni changamoto kubwa kwetu. Nina hakika tutaifanya."

Matokeo ya mechi ya juzi Jumapili ni mwendelezo wa matokeo mabaya kwa United baada ya kushindwa katika mechi tano mfululizo.

Mara ya mwisho United walijikuta katika hali hiyo ilikuwa kati ya Novemba na Desemba mwaka 2015 ambapo walicheza mechi nane bila kupata ushindi chini ya Kocha, Louis van Gaal.

Matokea hayo sasa yanamaanisha kwamba, vijana wa Ole Gunnar Solskjaer hawana nafasi ya kuifikia Chelsea au Tottenham na wana nafasi finyu ya kuiondoa Arsenal katika nafasi ya tano.

Alexis Sanchez pia huenda asicheze katika mechi ya mwisho kati ya United dhidi ya Cardiff itakayochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford, baada ya kujeruhiwa katika kipindi cha pili cha mechi ya iliyopita dhidi ya Huddersfield.

Huddersfield ambao wako chini kabisa katika jedwali la msimamo wa ligi wakiwa na pointi 11, wanatarajiwa kuchuana na Southampton Jumapili ijayo.

Sanchez alipewa nafasi ya kuanza mechi kwa mara ya kwanza tangu Machi 2 mwaka huu baada ya washambuliaji wenzake Romelu Lukaku na Anthony Martial kuumia.

Macho yote sasa yanamwangazia kiungo huyo raia wa Chile kabla ya mwisho wa msimu huu baada ya Solskjaer kuahidi kufanyia marekebisho makubwa kikosi chake.

Inasadikiwa kuwa mshahara wa Sanchez hausaidii United kushauriana kuhusu mkataba wa wachezaji kama David de Gea, Juan Mata na Ander Herrera.

De Gea, pia amekuwa akikosolewa vikali kutokana na kiwango chake katika mechi kadhaa zilizopita.

## ZISIKUPITE

### SPURS YAKUBALI YAISHE

KLABU ya Tottenham imeanza kujiandaa kuishi bila ya kiungo wake raia wa Denmark, Christian Eriksen, na ikiwa katika hatua za mwisho za kumnasa nyota wa Ajax, Donny van de Beek (22), ambaye pia anawaniwa na Real Madrid pamoja na Bayern Munich. ***(Mirror)***

### SARRI AMTAKA HIGUAIN

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri, ameitaka klabu hiyo impe mkataba wa kudumu straika wa Argentina, Gonzalo Higuain, ambaye alikuwa kwa mkopo akitokea Juventus ili kukiimarisha kikosi chake. ***(Goal.com)***

### WELBECK SAFARI IMEIVA

MSHAMBULIAJI wa zamani wa England, Danny Welbeck (28), hatapewa mkataba mpya na Arsenal na kwa maana hiyo atakuwa mchezaji huru wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto. ***(Sky Sports)***

### MODRIC KUONDOKA MADRID

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, anatarajia kumpa ruhusa ya kuondoka klabuni hapo nyota, Luka Modric baada ya kutokuwa katika kiwango cha juu kutokana na umri wake kufikia miaka 33. ***(AS)***

### NYOTA CITY MTEGONI

WACHEZAJI wa Manchester City watagawana motisha ya pauni milioni 15 kama watafanikiwa kutetea taji la ubingwa wanalolishikilia. ***(Telegraph)***

### WACHEZAJI UTD YAWAKUTA

IDADI kubwa ya wachezaji wa Manchester United watakatwa robo ya mishahara yao kutokana na timu hiyo kushindwa kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(Mail)***

### LOZANO, TRIPPER SOKONI

KOCHA Carlo Ancelotti, amethibitisha kuwa Napoli inataka kumsajili mchezaji wa PSV, Hirving Lozano (23) na beki wa Tottenham, Kieran Trippier. ***(Goal)***

### SILVA, SANSON WAWINDWA

WOLVES imeweka wazi kuwa na mpango wa kumsajili straika wa AC Milan, Andre Silva na kiungo wa Marseille, Morgan Sanson ndiyo nyota muhimu inaowahitaji. ***(Birmingham Mail)***

### RONDON - NIKO VIZURI

STRAIKA wa West Brom, Salomon Rondon (29), ambaye yuko kwa mkopo katika kikosi cha Newcastle ameitaka klabu hiyo kumsajili na kutohofia umri wake huku akisema anazidi kuimarika kama ubora wa mvinyo unavyoongezeka. ***(Mirror)***

### MORENO KUMVUTA FERNANDES

MANCHESTER City inapanga kumtoa kwa mkopo Marlos Moreno kwenda Santos Laguna, kama sehemu ya kumnasa kiungo wa Sporting, Bruno Fernandes (24). ***(Sport Witness, via Manchester Evening News)***

### ZOUMA KUREJEA CHELSEA

BEKI wa Chelsea, Kurt Zouma, ambaye alikuwa kwa mkopo Everton, anatarajia kurejea Stamford Bridge mapema kuanza maandalizi ya msimu mpya, ingawa Toffees imeonyesha nia ya kumpa mkataba wa kudumu Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Liverpool Echo)***

## HABARI MICHEZO

# MSOLLA- YANGA ITASHINDA MICHEZO YOTE ILIYOBAKIA

**Na Somoe Ng'itu**

MWENYEKITI mpya wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla, amesema kuwa kazi ya kwanza atakayoifanya katika klabu hiyo ni kuhakikisha Yanga inapata ushindi katika mechi zote zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

**Yanga ndio inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 80 baada ya kucheza mechi 34, kwa maana hiyo imebakiza michezo minne ili kumaliza msimu wa mwaka 2018/19.**

Msolla aliibuka mshindi katika nafasi hiyo baaada ya kupata kura 1,276 wakati mpinzani wake Tiboroha, aliambulia kura 60 katika uchaguzi huo uliofanyika juzi kwenye Ukumbi wa Bwalo la Polisi Oysterbay jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kuchaguliwa, Dk. Msolla, ambaye alikuwa kocha wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), alisema kuwa anataka kuona klabu hiyo inamalizika kwa heshima na kutwaa ubingwa wa ligi hiyo ambao unashikiliwa na watani zao, Simba.

Msolla alisema kuwa yeye pamoja na viongozi wenzake watashirikiana kuhakikisha kila kitu kinakwenda vema ndani ya klabu hiyo katika kipindi cha miaka minne watakayokaa madarakani.

"Jambo la kwanza na muhimu ni kumsaidia Mwinyi Zahera aweze kupata fedha zote ambazo anazitaka ili aweze kusajili kikosi imara kwa ajili ya msimu ujao, nimeshangazwa na kufurahishwa na idadi nyingi ya kura nilizozipata," alisema Dk. Msolla.

Alisema pia chini ya uongozi wake watajipanga kuhakikisha timu yao ya wanawake ya Yanga Princess inamaliza vizuri mechi zake za Ligi Kuu Wanawake Tanzania.

"Kwanza napenda niwaambie wachezaji tupo pamoja, tunajipanga kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri," alisema kiongozi huyo na kuahidi kuanza safari ya kwenda kuishangilia timu yake ambayo jana ilikuwa ugenini dhidi ya Lipuli FC katika mchezo wa hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA.

Baada ya mechi ya jana kumalizika, Yanga itasafiri kuelekea Musoma kuwafuata wenyeji Biashara United kwa ajili ya mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao utachezwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume.



Mwenyekiti mpya wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla (kushoto), akiangalia jambo katika simu yake pamoja na aliyekuwa mpinzani wake, Dk. Jonas Tiboroha, muda mfupi kabla ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa Yanga uliofanyika juzi jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

# Prisons yalia kukosa bahati

**Na Mwandishi Wetu**

KUKOSA umakini na umaliziaji mbovu ni baadhi ya sababu zilizochangia timu ya Tanzania Prisons kufanya vibaya katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Simba iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Tanzania Prisons ililala bao 1-0 katika mchezo huo ambao uliwafanya mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba wafikishe pointi 78, mbili nyuma ya vinara Yanga.

Ezekia Mwashilindi, alisema baada ya mechi hiyo kuwa, kikosi chao hakikutumia vema nafasi walizozitengeneza tofauti na wapinzani wao Simba ambao waliitumia vizuri nafasi hiyo moja ambayo ilizaa bao.

"Kusema kweli tulitengeneza nafasi nyingi, hatukuwa makini katika kumalizia, mastraika wengi hawakuwa watulivu, tulitengeneza nafasi nyingi lakini tulizipoteza, Okwi (Emmanuel) alitumia nafasi ile moja na kufunga," alisema Mwashilindi.

Hata hivyo nyota huyo alisema kuwa walicheza kwa kuwaheshimu Simba ambao walicheza kwa bidii zaidi kwa sababu walihitaji ushindi ili kuendeleza mbio zake za kutetea ubingwa wanaoushikilia.

Naye Kocha wa Prisons, Adolf Rishard, aliwataka wachezaji wake waache "kupaki basi" na kwenda kushambulia, katika kipindi cha pili ili kuwasumbua Simba.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 34 | 25 | 5 | 4 | 54 | 24 | 80 |
| 2. Simba | 30 | 24 | 3 | 2 | 61 | 12 | 78 |
| 3. Azam | 33 | 19 | 9 | 5 | 49 | 20 | 66 |
| 4. Mtibwa Sugar | 33 | 14 | 6 | 13 | 34 | 26 | 48 |
| 5. Lipuli | 34 | 12 | 12 | 10 | 30 | 31 | 48 |
| 6. Singida Utd | 34 | 11 | 10 | 13 | 26 | 33 | 43 |
| 7.Ndanda | 32 | 11 | 10 | 11 | 22 | 30 | 43 |
| 8. KMC | 33 | 9 | 15 | 9 | 33 | 25 | 42 |
| 9. TZ Prisons | 34 | 10 | 12 | 12 | 26 | 26 | 42 |
| 10. Coastal Union | 33 | 9 | 14 | 10 | 29 | 33 | 41 |
| 11. Mbeya City | 32 | 11 | 7 | 14 | 31 | 34 | 40 |
| 12. Kagera Sugar | 33 | 9 | 12 | 12 | 28 | 35 | 39 |
| 13. JKT Tanzania | 33 | 9 | 12 | 12 | 20 | 28 | 39 |
| 14. Ruvu Shooting | 34 | 9 | 12 | 13 | 31 | 40 | 39 |
| 15.Stand United | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 16. Alliance | 34 | 9 | 11 | 14 | 26 | 38 | 38 |
| 17. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 18. Biashara United | 33 | 9 | 10 | 14 | 25 | 31 | 37 |
| 19. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# *Tiboroha afunguka alijua atashindwa*

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI aliyekuwa mgombea wa nafasi ya uenyekiti katika uchaguzi wa Yanga, Jonas Tiboroha, amesema kuwa yuko tayari kufanya kazi na mwenyekiti mpya, Mshindo Msolla, ameeleza kwamba alifahamu hatashinda katika kinyang'anyiro hicho.

Akizungumza na gazeti hili jana, Tiboroha, alisema kuwa kama Yanga itaona anaweza kutoa mchango wake katika kufikia malengo, wasisite kumpatia majukumu yoyote kwa sababu yeye bado ni mwanachama wa klabu hiyo.

Tiboroha alisema kuwa amekubaliana na matokeo hayo ambayo anadai aliyajua mapema kabla ya wanachama hawajaanza mchakato huo wa kupiga kura.

"Nilijiua mapema matokeo haya," alisema kwa kifupi Tiboroha wakati wagombea wengine wa nafasi hiyo, Mbaraka Igangula na Elias Mwanjala waliamua kujitoa.

Alisema kuwa anaomba wanachama wajumuike pamoja kushirikiana na uongozi ili kuifanya Yanga isonge mbele na huu ni wakati wa kuvunja makundi yaliyokuwapo wakati wa kampeni za uchaguzi.

"Napenda nitoe shukrani zangu kwa kamati ya uchaguzi, pili nawashukuru wapiga kura wote, hakika Wana- Yanga mmeongea kwa sauti kubwa sana," alisema Tiboroha.

Aliongeza kuwa anampongeza mwenyekiti huyo mpya na kumtakia kila la heri katika utendaji wa kazi zake na anaamini atafanikiwa kuipeleka Yanga "kwenye nchi ya ahadi." Naye Fredrick Mwakalebela, Katibu Mkuu wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti baada ya kupata kura 1,206 na kuwashinda wapinzani wake akiwamo Janneth Mbene aliyepata kura 61, Titus Osoro (17), Yono Kevela (31) na Magege Chota aliyeambulia kura 12.


Walioshinda nafasi ya ujumbe ni Hamad Islam, Domonick Ituke, Kamugisha Kalokola, Saad Khimji, Salum Rupia, Rodgers Gumbo na Bahati Mwaseba.

# Michezo

Jumanne Mei 7, 2019
Nipashe



Pjanic afikiria kwenda PSG HABARI UK.29




Mshambuliaji wa Manchester United, Alexis Sanchez (kushoto), akifanyiwa faulo na beki wa Huddersfield Town, Christopher Schindler katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa Jumapili jioni kwenye Uwanja wa John Smith. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

## Ndoto za Yanga Afrika zayeyuka

**Na Adam Fungamwango**

NDOTO za Yanga kushiriki mashindano ya kimataifa kupitia michuano ya Kombe la FA Tanzania imefutika baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Lipuli FC katika mchezo wa hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA uliochezwa jana kwenye Uwanja wa CCM Samora mjini Iringa.

Kwa matokeo hayo, sasa Lipuli FC inaungana na Azam FC kutinga fainali za mashindano hayo zitakazochezwa mapema mwezi ujao kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi. Azam FC yenyewe ilifuzu hatua hiyo baada ya kuifunga KMC ya jijini Dar es Salaam katika mchezo mwingine wa hatua hiyo uliochezwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini.

Bao la kwanza la Lipuli lilipatikana dakika ya 27 kupitia kwa straika wake tegemeo, Paul Nonga baada ya kutokea piga nikupige kufuatia mpira uliotemwa na kipa wa Yanga, Klaus Kindoki.

Wenyeji hao waliendelea kupambana katika mchezo huo ulioanza saa 9:30 mchana na walifanikiwa kufunga bao la pili baada ya shuti la Nonga kutemwa na kipa Kindoki, kilitokea kizaazaa golini na Daruweshi Saliboko kuuweka wavuni dakika ya 38.

Mabao hayo ya Lipuli yalidumu mpaka dakika 90 za mchezo huo zilipomalizika na kuwafanya watinge fainali za michuano hiyo kwa mara ya kwanza msimu huu.

Lipuli ilianza kwa kulisakama lango la Yanga na dakika ya 15, ilikosa bao kwa mpira wa faulo uliopigwa na Haruna Shamte ukatemwa na kipa Claus Kindoki, lakini washambuliaji wake walishindwa kuukwamisha wavuni.

Heritier Makambo aliyekuwa hatari kwenye kipindi cha kwanza, hakuweza kufurukuta katika kipindi cha pili, badala yake Amissi Tambwe aliyeingia kipindi cha pili, ndiye aliyekuwa hatari kwenye lango la Wanapaluhengo.

# Simba yarejesha ‘Do or Die’ Bara

## Ni katika kusaka pointi 15 ili wafanikishe malengo ya kutetea ubingwa wa Ligi Kuu...

**Na Somoe Ng'itu**

UONGOZI wa Klabu ya Simba ya jijini Dar es Salaam, umesema kuwa wanarejea kutumia kampeni yao ya 'Do or Die' ambayo waliitumia katika mechi za mashindano ya kimataifa za Ligi ya Mabingwa Afrika sasa imehamia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa ajili ya kusaka pointi 15, imeelezwa.

**Mabingwa hao watetezi wenye pointi 78 baada ya kucheza mechi 30, wamebakiza michezo nane ili kumaliza msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara mwaka 2018/19 wakati vinara wa ligi hiyo, Yanga ambao wana pointi 80 wamebakiza michezo minne.**

Endapo Simba itapata ushindi wa mechi tano kati ya hizo zilizosalia, itafikisha pointi 93 ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine yoyote inayoshiriki ligi hiyo msimu huu, wakati Yanga ikishinda michezo yake yote iliyosalia itafikisha pointi 92.

Akizungumza jana jijini, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema kuwa lengo la kutumia kampeni hiyo ni kuhakikisha wanavuna pointi hizo na kutetea ubingwa wa ligi hiyo ambao bado wanaushikilia. Manara alisema kuwa ili waweze kutimiza malengo hayo, wanahitaji mashabiki wa timu hiyo wajitokeze kuishangilia timu yao kama walivyofanya katika michezo ya kimataifa ambayo walishiriki msimu huu.

"Tuna mechi tano mfululizo Dar es Salaam, pointi 15 za Dar es Salaam ni lazima tuzichukue, mikoani kuanzia Mwanza, Musoma, wametuunga mkono sana, mara nyingi sisi tumekuwa tukiujaza uwanja katika mechi za kimataifa, kampeni yetu ni kuhakikisha tunajitokeza kwa wingi, tunawaomba Wana-Simba wajitokeze kwa wingi, katika mechi tano, tuanze Jumatano, kama tunaweza kuujaza Uwanja wa Taifa, hatushindwi kwenye Uwanja wa Uhuru ambao unaingiza watu 15,000 hadi 20,000. Tunahitaji tushinde, wala hatutajali matokeo ya Yanga," alisema Manara.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa kikosi chao kimerejea salama kutoka Mbeya na kitaanza mazoezi leo kwa ajili ya kuikaribisha Coastal Union kutoka jijini Tanga kwenye mchezo mwingine wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa kesho.

Mechi nyingine zitakazofuata za Simba za ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ni dhidi ya Kagera Sugar itakayocheza Ijumaa, Azam FC (Mei 13), Mtibwa Sugar (Mei 16) na dhidi ya Ndanda FC kutoka Mtwara itakayochezwa Mei 19 mwaka huu, zote kwenye Uwanja wa Uhuru.

Simba ambayo msimu huu ilifika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kutolewa na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), itacheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Sevilla ya Hispania na itafunga pazia la Ligi Kuu kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro kwa kuvaana na wenyeji, Mtibwa Sugar.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >